ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita – Tarehe 27 Mei, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya Kamati ya kusimamia Viongozi wakuu wa Kitaifa, kuhusiana na Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2016/2017.

Nam. 98

Kufanyika kwa Uchaguzi mara mbili Zanzibar

Mhe. Yussuf Hassan Iddi– Aliuliza**:**

Kwa kuwa nchi yetu imefanya uchaguzi mara mbili na kupelekea kuingia hasara kubwa kwa kipindi kifupi.

a) Je, wale waliotia hasara Serikali imechukua hatua gani.
b) Je, Serikali imejipangaje kuona kuwa hali ile haijirudii tena katika chaguzi zinazokuja.
c) Je, Serikali haioni haja ya kuletwa Barazani Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya mwaka 1984 ili iendane na mazingira na wakati ulivyo sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali inaendelea kufanya uchunguzi na wale wote walioshiriki kuharibu Uchaguzi hatua za Kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha Mhe. Spika, Serikali ilitimiza wajibu wake wa kuipatia Tume ya Uchaguzi fedha za kufanikisha Uchaguzi wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016. Uchaguzi huo umefanyika kwa mafanikio makubwa na sasa tumepata viongozi waliochaguliwa na wananchi wenyewe kwa uhuru na haki.

(b) Mhe. Spika, katika kuhakikisha matatizo yaliyojitokeza katika Uchaguzi wa Oktoba 2015 hayajirudii tena, serikali itaifanyia marekebisho Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya 1984, ili kuweka misingi bora ya uteuzi wa watendaji wote wa uchaguzi, ikiwemo sifa za muombaji kuanzia Wasimamizi wa Majimbo, Wasimamizi wa vituo, Wasaidizi wasimamizi wa vituo pamoja na waongozaji mistari. Sambamba na hilo serikali itahakikisha inasimamia utekelezaji wa sheria hiyo husika kwa kuteua watendaji wenye sifa zinazotakiwa.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika kifungu (b) kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Tume ya Uchaguzi Zanzibar imeona ipo haja kwa Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya 1984 kufanyiwa marekebisho ili iendane na wakati. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, kwa kuwa jibu lake mama Mhe. Waziri amesema hadi leo uchunguzi haujakamilika na toka umalizike Uchaguzi huu uliofutwa wa Oktoba 25 hivi sasa takriban ni mwezi wa 7. Je, ni lini uchunguzi huo utakamilika.

(b) Kwa kuwa chanzo cha hasara ya uchaguzi uliopita imesababishwa sana na wasimamizi uchaguzi wa majimbo kwa kukosa uzalendo na uaminifu. Je, serikali haioni haja ya wasimamizi hao wa uchaguzi wa majimbo wakaajiri kama walivyoajiriwa maafisa wa uchaguzi wa wilaya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

(a) Mhe. Spika, uchunguzi huu haukuwagusa tu wale wasimamizi wa Tume ya Uchagizi, bali wamo wengi walioshiriki katika kuharibu uchaguzi huu. Kwa hivyo, kila aliyefanya kosa jambo hili itabidi limguse. Kwa hivyo, uchunguzi unafanywa kwa kina wapatikane wahusika na mara uchunguzi utakapokamilika basi hatua rasmi za

kisheria zitachukuwa mkondo wake ili kila aliyefanya kosa ashitakiwe kwa mujibu wa makosa yake.

Naomba sana Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe tuvute subira, kazi hii ifanyike vizuri, chungu kipo jikoni!

(b) Kuhusu uajiri wa wasimamizi wa majimbo, kwa kuwa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Tume na tunafanya utaratibu wa kuona namna gani tutabadili sheria yetu ili ioane na wakati wa leo. Ushauri wako tutaufanyia kazi tuone namna gani tutakavyoweza kusaidia, kwa sababu nia na dhamira ni kuwa na sheria nzuri itakayokidhi haja, itakayoondoa matatizo ambayo yamejitokeza. Lakini niseme wazi matatizo mengine sio sheria, matatizo mengine ni tamaa binafsi.

Kwa hiyo, wale ambao tunawapa hizi kazi za kufanya lazima kama ulivyosema wawe wazalendo, wawe waaminifu kwa nchi yao na wawe tayari kuishughulikia nchi yao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba Waheshimiwa Wawakilishi tuwe na subira uchunguzi unafanywa, lakini nataka kumwambia kwamba subira ina mwisho wake.

(a) Uchunguzi huu utaendelea mpaka lini wakati tunaona wachafuzi hawa waliosababisha kuchafua uchaguzi wanaenda na kurudi makazini mwao na huku wakitoa maneno machafu juu ya serikali hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, subira ina mwisho itafika mwisho wake. Lakini napenda nieleze Baraza lako tukufu kwamba uchunguzi unafanywa kwa makini sana, na Waheshimiwa Wajumbe mnajua kwa kina nini kimetokea. Ilikuwa dhamira ya makusudi ya kuuharibu uchaguzi huu kwa sababu za tamaa za watu fulani ya kutaka madaraka, na mnaona hali mpaka leo ya chini ya kuharibu utulivu wa nchi uliopo kuharibu amani yetu tuliyonayo, kuharibu mafanikio makubwa ya maendeleo ya nchi yetu yakiendelea kwa chini chini.

Kwa hivyo, kazi kubwa ipo mbele yetu sote na ndio maana nataka nichukue fursa hii kuvipongeza sana vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa hatua wanazochukua katika kuhakikisha kwamba amani inalindwa.

Napenda nitoe wito kwa wananchi wale ambao wanapenda kuingilia mambo wasiyoyajua au kufuata shangwe litakalowakuta shauri yao. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Spika, kwa kuwa uchaguzi umekwisha lililobakia ni wananchi kushirikiana na viongozi ili kuleta maendeleo. Lakini mpaka leo hii kuna watu wanapita kila kijiji kuhamasisha watu wafanye migomo. Je, kwa nguvu uliyonayo wewe, na kwa kuwa Ramadhani imekaribia, na kwa kuwa asilimia 95 ya Zanzibar ni waislamu, je, wizara yako ina mpango gani wa kukomesha habari hii kabla ya kufika mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba Mhe. Said Omar Said arudie swali lake vizuri kwa kuzungumza na *mic* ili apate majibu sahihi.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Spika, kwa kuwa uchaguzi umekwisha lililobakia ni wananchi kushirikiana na viongozi wa serikali ili kupatikana maendeleo ya Zanzibar. Lakini hata hivyo mpaka muda huu kuna viongozi wanapita nyumba hadi nyumba, mtaa, kila mtu ili kuhamasisha watu wafanye mgomo katika huduma za kijamii na za kidini, na hili ni miongoni mwa mambo anayoyachukia sana Mwenyezi Mungu. Na kwa kuwa karibuni tu kesho kutwa tunategemea kufunga mwezi wa Ramadhani, na kwa kuwa asilimia 95 ya Wazanzibari ni waislamu ili tusije tukapata janga jengine kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa migomo hii, wizara yako ina mpango gani wa kuondosha au kusimamisha migomo hii kabla ya kuingia Ramadhani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika sasa nimemfahamu vyema kabisa Mhe. Said Omar Said na naomba nimjibu swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyosema uchaguzi umekwisha na uchaguzi mwengine ni mwaka 2020, serikali imeundwa na mambo yanakwenda sawa, na yoyote yule mwenye dhamira mbaya anayekusudia kuharibu amani ya nchi, anayekusudia kuwapotosha wananchi, huyo mkondo wa sheria utachukua nafasi yake.

Nataka niwaambie wananchi wote kwamba serikali haidhihakiwi. Kwa hiyo, anayedhihaki serikali naye itamdhihaki, kwa sababu sheria ziko wazi na zitachukua mkondo wake. Hivyo basi, nataka niwahakikishe Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu imeanza kuchukua hatua mbali mbali za kuelimisha wananchi ili waelewe umuhimu wa amani waelewe upotoshaji unaoendelea, na waelewe misingi ya kuheshimu sheria za nchi yetu, hususan katika kipindi ambacho tunaelekea mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Hata hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Said Omar Said na Waheshimiwa Wawakilishi leo hii tunasoma Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mambo haya yataelezwa kwa kina. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Nam. 82

Kuanzishwa kwa Maghala ya Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said:– Aliuliza**:**

Suala la biashara hasa biashara muhimu za vyakula kama vile mchele, unga na sukari hivi sasa imeachwa huru kwa wafanyabiashara binafsi. Hatua hii inaweza kutumika vibaya kwa wafanyabishara wasio waaminifu na wahujumu wa uchumi wa Taifa hasa katika vipindi vya uchaguzi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Maghala yake wenyewe ya kuhifadhi chakula ili kujikinga na hali kama hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na taratibu za matayarisho ya uanzishaji wa Hifadhi ya Chakula ambayo lengo la kuanzishwa kwake ni kuhifadhi chakula cha akiba kwa ajili ya kuikinga nchi na janga la njaa. Chakula kitakachohifadhiwa ni mchele, ambao ni chakula kikuu kwa Zanzibar. Akiba hii ya chakula itakuwa ikitumika kwa ajili ya kudhibiti ongezeko kubwa la bei ya mchele na kutoa chakula kwa watu waliokabiliwa na majanga ya njaa kwa utaratibu maalum.

Mhe. Spika, katika matayarisho haya ya hifadhi ya chakula, serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tayari imeshakamilisha mambo yafuatayo:-

- Muongozo na taratibu za kusimamia na kuendesha hifadhi ya chakula.
- Muongozo wa viwango vya ubora wa mchele na mpunga utakaonunuliwa kwa ajili ya hifadhi ya chakula;
- Kanuni za kusimamia uendeshaji wa hifadhi ya chakula; na
- Ukarabati wa ghala moja kati ya mawili ya hifadhi hiyo.

Mhe. Spika, mipango ya serikali ni kuanzisha rasmi hifadhi hii ya chakula katika mwaka ujao wa fedha 2016/2017 na katika kipindi hicho inapanga kutekeleza yafuatayo:-

- Ununuzi wa vifaa vya hifadhi ya chakula (ikiwemo mizani, vifaa vya ofisi na vifaa vya ukaguzi wa ubora wa chakula);
- Kutoa mafunzo kwa watendaji wa hifadhi ya chakula;
- Ununuzi wa mchele kwa ajili ya hifadhi.

Mhe. Spika, pamoja na umuhimu wa kuwa na chakula lakini ni vyema kwa wananchi kujifunza kuweka akiba pale wanapopata ziada iwe ya chakula au ya fedha ili janga linapotokea wawe na pa kuanzia na serikali ichangie upungufu utakaojitokeza.

Mhe. Spika: Ahsante kwa majibu. Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa swali la nyongeza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, kwa historia yangu naona kwamba Zanzibar kilimo cha mpunga ni cha muda mrefu sana, lakini mpaka leo sijawahi kumuona hata mtu mmoja akivuna mpunga akapata hata gunia moja la kuuza.

a) Je, serikali ina mpango gani wa kuweza kuwawezesha wananchi wa kilimo cha mpunga ili waweze kupata chakula na sehemu nyengine ya kuuza.

b) Serikali ina mpango gani kwa sababu tokea asili mbegu zao ni za mwaka kwa mwaka, kama vile sijui Kiangalawa, Jeuri Sitaki ambao ni mbegu ya mpunga wa zamani. Sasa kuna mpunga wa kisasa wa miezi mitatu au miezi miwili. Kwa msimu ni mara tatu unaweza ukavuna na ukauza. Je, serikali ina mpango gani wa kubadilisha mbegu hizi tukapata chakula cha haraka cha faida na kuuza.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la pili nitaomba alirejee lakini kwa sababu ninamjibu la (a).

(a) Mhe. Spika, wakulima wanaolima kilimo cha mpunga cha umwagiliaji maji wanapata magunia au tuseme wanapata mazao mengi sana na siyo gunia moja haliwatoshi. Wanapata mazao mengi sana kupitia kilimo cha umwagiliaji maji na kilimo pia cha *rainfall*. Tofauti ni kwamba umwagiliaji maji wanavuna mavuno mengi zaidi.

Sasa sijamuelewa yeye anasema kwamba anapata gunia moja, hawezi ku-*save*, hapo sijamuelewa labda angeliweka sahihi zaidi.

Mhe. Spika: Mhe. Suleiman Sarahan hebu liweke sawa kwa Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, swali la (b) anasema hajalisikia ni kwamba, kikawaida mpunga wetu ni ule ule ambao tumeuzoea kama tunalima ambao unachukua muda mpaka kuvuna kama miezi sita. Lakini sasa hivi katika nchi nyingi tu kuna mpunga ambao miezi mitatu wakulima wanavuna, na kilimo chake ni sehemu ndogo lakini kina tija zaidi.

Je, serikali ina mpango gani wa mbegu hizo kuwasaidia wakulima wa kwetu na kuweza kupata tija ya chakula na kuuza.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said. Kwanza swali mama linasema suala la ghala na siyo suala la mbolea au la mbegu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe ngoja asaidie.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea...

Mhe. Spika: Waheshimiwa *order* kidogo, tumsikilize Mhe. Waziri akitupa majibu. Endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu kwa maswali mawili ya nyongeza aliyouliza Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo.

(a) Kwanza wakulima wetu kwa kweli wamebadilika sana, na kwa sasa hivi kilimo cha juu wanazalisha *0.9 per hectare*. Hilo ni ongezeko kubwa kutoka pale walipokuwepo, lakini kwa kilimo ambacho wanamwagilia maji wanatoa mpaka *tons* tatu mpaka tatu na nusu kwa hekta moja. Kwa hivyo naona kuna mabadiliko makubwa sana kwa wakulima.

Lakini jambo la kufurahisha zaidi Mhe. Spika, ukienda leo kwa mfano kwenye bonde la Cheju unamkuta mkulima ana mashamba ya aina mbili. Shamba moja la biashara na shamba moja la chakula. Kule kwa

kumwagilia maji ni kwa biashara na wanaiuzia serikali. Kuna wakulima wanadai mpaka laki tisa hivi sasa. Hii ni kuonesha kwamba wana *surplus* ya kuiuzia serikali. Halafu wana chakula chao ambacho wanalima mashamba ya juu, wana akiba ya chakula. Kwa hivyo ni kweli kabisa kutokana na taaluma tulizozitoa za kilimo na pembejeo zilizotolewa na serikali, asilimia zaidi ya 80 za pembejeo wanaopewa na serikali bure zimewasaidia wakulima kuweza kulima vizuri.

(b) Kuhusu mbegu ni kweli kabisa tunawapa mbegu wakulima walime, mbegu ambazo inanunua serikali. Na ndiyo maana wakulima wanaidai serikali kwa sababu tumewapa mbegu nzuri walime halafu waiuzie serikali. Serikali inanunua kwa bei ya elfu moja mia mbili; wao tukiwauzia mbegu tunawauzia kwa shilingi mia mbili tu. Hii ni kuonesha kiasi gani serikali inavyotoa umuhimu wa kusaidia wakulima waweze kuzalisha ili tupate kipato kikubwa.

Kwa hivyo siyo kweli kama hawana mbegu nzuri. Wanazo mbegu nzuri, wanazalisha, wanapewa na serikali zile mbegu wazizalishe. Halafu serikali inanunua katika katika kuwasaidia wao kupata mapato zaidi. Kwa hivyo *programme* ni nzuri na kama hekta 34 elfu za juu ukizilima, tunaweza tukazalisha *tons* 78,000 za mchele. Mahitaji ya mchele hapa ni *tons* 80,000 kwa mwaka. Tukizalisha hekta za juu na zile 8,500 za *irrigation*, tutaweza kujitosheleza kwa chakula bila wasi wasi wowote Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante kwa majibu yako Mhe. Waziri. Na Mhe. Shadya Mohammed Suleiman nimekuona kwa swali la nyongeza na mwisho kabisa Mheshimiwa nyuma kule. Mhe. Shadya.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mpango gani juu ya suala zima la ghala liliopo Pondeani kwenye Kijiji cha Chake Chake wakati ghala hiyo kuna mzozo kwamba ghala hiyo kapewa mtu kwa ajili ya kuhifadhia pombe.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Shadya kwa kuwa sasa tumeshalifanyia ukarabati ghala la Malindi na badala yake tutalifanyia ukarabati ghala lililokuwepo Chake Chake Tibirinzi kwa ajili ya kuhifadhia chakula.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika: Swali moja lenye (a) na (b).

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri umeeleza kwenye swali lako mama kama kuna maghala Unguja na Pemba.

(a) Ni maghala mangapi yaliopo Mikoa miwili ya Pemba.

(b) Mwaka 1984 Unguja na Pemba kulijengwa maghala lakini sasa hivi maghala yale yote yameshakuwa mabovu. Je, una mpango gani wa kuweza kuyatengeneza maghala haya ili yaweze kutumika kwa ajili ya kuwekea mbegu pamoja na nafaka nyengine za kilimo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe atajibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba yapo maghala na yamedumu kwa muda mrefu na mengine yameharibika. Sasa hivi serikali kwenye *programme* tuliyonayo na *FAO* ni kutengeneza maghala yote ambayo yapo chini ya wizara yetu kwa ajili ya kuhakikisha kabisa yanaweza kuhifadhi chakula na vile vile kutumika kwa nafaka nyengine. Kama munavyofahamu Baraza lilipitisha sheria kwamba vile vile *ZSTC* inunue na nafaka nyengine. Tunategemea maghala tuliyonayo sisi waliyonayo *ZSTC* kwa pamoja tunaweza kukidhi mahitaji ya kuweka akiba ya chakula au aina zote za mazao yatakayozalishwa.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 37 Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis aliuliza maghala mangapi yaliyokuwepo Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa hivyo hakupata idadi ya maghala mangapi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana. Ni suala la takwimu itabidi tumletee takwimu.

Nam. 39

Ucheleweshwaji wa Kupatikana Viwanja kwa Wananchi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Kumekuwepo na malalamiko ya miaka mingi kwa wananchi kuhusu urasimu wa upatikanaji wa viwanja kwa ujenzi wa makaazi na kusababisha watu wengi kujenga katika maeneo yasiyo salama na kujenga kiholela.

a) Kwa nini Serikali inashindwa kupima viwanja vya kutosha na kuwapatia wananchi ili kuondoa tatizo la ujenzi wa nyumba mabondeni na kuwa chanzo cha kuhatarisha usalama wao kila mvua zinaponyesha.

b) Mwananchi kusubiri kiwanja miaka 10 hadi 20 bila ya mafanikio, Serikali haioni kuwa inamrudisha nyuma kimaendeleo mwananchi.

c) Ni viwanja vingapi vinatarajiwa mpaka sasa kupimwa na kupewa wananchi na maombi ya watu ambao hawajapata mpaka sasa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi ambaye pia ni Mbunge Mteule swali lake Nam. 39 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kumekuwa na malalamiko juu ya ugawaji na upimaji viwanja. Malalamiko haya ni ya msingi kwani kila mwananchi ana haki ya msingi ya Kisheria kupata makaazi salama. Lakini, Serikali haijashindwa kupima viwanja. Inachokifanya Serikali ni kutafuta jawabu la kudumu la mustakbali mzima wa maendeleo ya nchi na mahitaji ya wananchi katika makaazi.

Mhe. Spika, utafiti tuliofanya unatuonesha kuwa Zanzibar ni nchi yenye watu wengi katika eneo la mraba. Mpaka kufikia mwaka 2015

idadi yetu ni watu 610 katika kilomita ya mraba *(610 persons/km^2)* wenzetu Tanzania Bara wako watu 52 katika kilomita ya mraba *(52 persons/km^2).* Hii inamaanisha mambo mengi, lakini mojawapo ni kuwa, Zanzibar itakuwa na uwezo mdogo sana wa kuhakikisha kila mmoja wetu anakuwa na kiwanja chake, ili ajenge peke yake, nyumba ya chini. Ili kutatua changamoto hiyo ya udogo wa ardhi, Serikali inajipanga kuhakikisha kila Mzanzibari anapata makaazi bora yenye bei nafuu na sio kila mmoja kupata kiwanja chake. Hili linawezekana.

Mhe. Spika, suala la ujenzi holela nalo limeshapatiwa ufumbuzi. Tayari Serikali imeshaanzisha Kamati ya Usimamizi na Udhibiti Ujenzi *(Development Control Unit – DCU),* kupitia Sheria ya Mipango Miji, ili kudhibiti ujenzi na kuhakikisha wananchi hawajengi katika maeneo yasiyofaa, na huhatarisha usalama wao. Kamati inakutana kila baada ya siku Kumi na Nne (14) na inafanya ukaguzi kila baada ya siku saba (7).

(b) Mhe. Spika, aidha, kwa vile Serikali inatilia mkazo sekta ya ujenzi wa nyumba, na kuwashajihisha wenye uwezo wajenge nyumba bora za bei nafuu, ili kila Mzanzibari apate makaazi bora, suala la kusubiri makaazi litaondoka. Na ili tupate kukaa wengi zaidi katika eneo moja. Tukumbuke kuwa, mwaka jana, Serikali iliunda Shirika la Nyumba kwa dhamira hiyo.

Aidha, mwaka 2010, Serikali ilipitisha Sheria ya Kondominia kwa kurahisisha ujenzi na ukodishwaji wa nyumba za ghorofa. Juhudi hizi naamini zitafanikiwa na wananchi hawatakuwa tena na sababu ya kusubiri miaka mingi kupata viwanja.

(c) Mhe. Spika, mwisho, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kugawa viwanja kwa mwaka huu.

Mhe. Spika, inachokifanya ni kupanga vizuri miji yake na kushajihisha ujenzi wa nyumba kwa Wawekezaji wa ndani na nje. Tayari Miji minne (Mji wa Zanzibar, Nungwi, Mkokotoni, Chwaka) imeshapangwa na mwaka huu Miji mengine mitatu (Chake Chake, Wete na Makunduchi) inatarajiwa kupangwa. Katika mipango hii maeneo ya ujenzi wa nyumba bora za bei nafuu yanapewa kipaumbele, kuondoa uhaba wa nyumba na kuondokana na dhana ya kusubiri viwanja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri.

Je, ni sababu gani watu wajenge kwenye mito na mikondo ya maji kama serikali imekuwa ikipima viwanja kwa madhumuni ya kuwapatia wananchi makaazi bora.

Na umesema katika suala lako ulipojibu mwaka huu hakuna mpango wa kutoa viwanja. Watu huko wanafuatilia viwanja ili wanataka kujua ni lini kama si mwaka huu, mwakani, mwaka 2020. Naomba utaje mwaka *specific,* ni mwaka gani tutapata viwanja.

La pili, ulipokuwa ukijibu swali la msingi kuwa umeanzisha Shirika la Nyumba na mkopo nafuu. Tumeshuhudia nyumba za maendeleo kama Michenzani, Kwa Mchina, nyumba zile wananchi hasa walengwa hazikuuzwa. Nyumba zile zimepewa na watu wakubwa wanaomiliki kuliko wale walengwa waliojengewa nyumba zile.

Je, unatoa kauli gani kwa suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza naomba tufahamu kwamba Wazanzibari wote ni walengwa. Na asiyepata kwa hapa basi atapata kwengine. Lakini tukija kwa nini wakati Kamati ipo na watu wanajenga pasipofaa ni kwamba ndiyo maana kukawa kuna sheria. Maana kama ingekuwa watu wote hawafanyi makosa kusingekuwa na sheria.

Sasa tunasema kwamba sheria itachukua mkondo wake, kwa sababu hii nchi inaendeshwa kwa sheria kama ambavyo Kifungu cha 5 cha Katiba ya nchi yetu inavyoeleza.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mwaka jana tulitoa viwanja. Muongozo wako Mhe. Spika, si maneno yangu mimi haya.

Mhe. Spika: Nimeshakuruhusu Mhe. Jaku usilalamike uliza hilo tatizo lako. Kiulize kiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nilipomuuliza katika swali la msingi alisema mwaka huu hatogawa viwanja. Mwaka gani atagawa viwanja. Hajajibu swali, kama mwaka 2020, 2030 ni lini.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku ninadhani kajibu hilo swali hata mimi nimesikia. Alisema hawana mpango wa kugawa viwanja mwaka huu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mwaka gani sasa anijibu.

Mhe. Spika: Ninadhani Mhe. Jaku iruhusu wizara ifanye kazi yake. Acha wizara wenyewe wakajipange na watakuja kutwambia. Bahati nzuri wizara haijapitisha bajeti yake. Wakati wa bajeti watajieleza hapa kwamba sasa hivi hatuna mpango wa kugawa viwanja na mpango tulionao utakuwa kwa mwaka gani. Wataeleza kwa urefu. (*Makofi*)

Kwa hivyo ninadhani Waheshimiwa Wajumbe baadhi ya haya maswali tusiyasukume sana kwa Mawaziri, tusubiri wakati wa bajeti zao. Tutapata muda wa nusu saa kabisa, utaeleza kila lililo lako. Halafu hapo tena kwenye vifungu utamshika mtu atakupa maelezo mazuri zaidi. Usisumbuke Mheshimiwa. (*Makofi*)

Nilimuona Mhe. Rashid Makame Shamsi na mwisho kabisa Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri kama hivi ifuatavyo.

Hivi karibuni serikali ilitoa tamko la kugawa viwanja ambao wamejenga katika eneo la mabonde na hivi sasa ni kadhia ya kila mwaka. Je, Mhe. Waziri anaweza kutwambia kwamba ni lini wananchi hawa watagaiwa viwanja hivyo, kwa sababu mvua nyengine za Vuli zinakuja.

Lakini je, vigezo gani vitatumika katika kugawa viwanja hivyo ukizingatia kwamba miaka ya nyuma kwenye maeneo haya haya waliondolewa na wakapewa viwanja vyengine.

Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Asiwe na hofu juu ya tamko la serikali. Serikali ikisema maana yake inatekeleza lakini kunakuwa na taratibu zake. Baada ya taratibu kukamilika kila tangazo litafanyiwa kazi ipasavyo.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kwa maelezo ya ziada ya kuongezea hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, licha ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongezee majibu ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli serikali ina mpango maalum wa kuhakikisha kwamba wale wananchi wanaoathirika mara kwa mara, kwa sababu ya mvua kubwa zinaponyesha ama kwa sababu wamejenga mabondeni au wamejenga katika njia zinazopita maji. Hivi ipo taarifa maalum ya wataalamu ambayo imekamilika na karibuni hivi itawasilishwa serikalini kufanyiwa kazi ili kuona hatua gani zitachukuliwa kwa wale wote wanaopata athari hizi kila mara.

Na utaratibu utakaotumika baada ya maamuzi ya serikali, vigezo vitakavyotumika ni wale ambao watakuwa waathirika wa kila mwaka. Wale ambao wamejenga katika maeneo ambayo njia za maji zinapita ama wamejenga mabondeni ama maeneo ambayo yanaingia maji mara kwa mara katika nyumba husika.

Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi ninakuomba uvute subra wakati serikali inalifanyia kazi jambo hili. Ninataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili na wananchi kwa jumla kwamba wale watakaohamishwa baada ya uamuzi wa serikali na wakapewa viwanja, basi nyumba zao wakati huo zitavunjwa baada ya kwishakuwepo na utaratibu maalum ambao wananchi hao wataelekezwa na serikali. Haitaruhusiwa kwa yeyote yule atakayepewa kiwanja na aina yoyote ya msaada atakaopewa na serikali kwa ajili ya ujenzi huo na akarejea katika maeneo hayo. Serikali haitovumilia tena kujengwa katika maeneo hayo. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kusubiri wakati serikali inalifanyia kazi jambo hili, ahsante sana.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa muongozo wako na pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri. Nakiri kwamba maelezo aliyotoa kuwa serikali iko kwa ajili ya wananchi wake na haitowabagua.

Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Tunguu ni katika eneo moja ambalo lilitajwa na Mhe. Rais katika mpango wa kujenga miji mipya, na viwanja vinakatwa kwa wananchi tofauti. Pia katika maeneo hayo ya Tunguu kuna watu wenye rika, madhehebu, dini lakini pia wenye asili ya Kibara. Na kumekuwa kuna hisia ya chini kwa chini kwamba viwanja vinapokatwa wananchi wenye asili ya Bara, wanakuwa wao wanapata khiyana kwamba wao ni watu wenye tabaka la pili na wanakosa viwanja. Lakini sambamba na hilo, kuna tatizo pia la eneo la kupata kwenda kuzikiana.

Je, Mhe. Naibu Waziri katika mpango mzima huo wa ukataji wa viwanja, unanihakikishiaje kwamba wananchi wangu katika Jimbo la Tunguu, ambao hao ni wenye asili ya Kibara utahakikisha na wao pia wanakuwemo katika huu mpango wa kukata viwanja?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, tunakubali kwamba mji ule umepangwa, na hilo suala alilosema la wale wenzetu wa asili ya Bara ambao anasema wako katika eneo lile wanatakiwa wafuate utaratibu, na utaratibu katika suala hili ni lazima waombe. Huwezi kutoka kwenda kumpa mtu kiwanja aliyekuwa hajaleta maombi, utaratibu upo, sheria zipo na raha yenyewe hii ni nchi ya Muungano, kwa hivyo hakuna mtu anayebaguliwa, ikiwa kuna mtu anaomba kiwanja kama anastahiki basi anapatiwa kiwanja chake, ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 56

Uharibifu Katika Mnara wa ZBC - Bungi

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kuuliza swali langu, naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Mbunge mstaafu wa CCM Jimbo la Mtambile na Katibu wa chama Mkoa wa Kusini Pemba Mhe. Saleh Juma kwa kufariki kwake ambako kumetokea jana, na maiti yake kusafirishwa kwenda Pemba na kuzikwa kijijini kwao Kwa Ngazo Kengeja. Kwa hivyo, natoa pole kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wote.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba swali langu namba 56 lipate majibu.

Kwa kuwa Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) linatumia mnara wa Bungi lakini kumejitokeza uharibifu mkubwa katika eneo la mnara wa kurushia matangazo Bungi, ikiwemo kuchimba mchanga katika maeneo hayo wakati eneo hilo ni muhimu kwa matangazo ya Redio.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuweka ulinzi ili kuunusuru mnara huo usije ukapata maafa zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 56, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, ni kweli kumejitokeza uharibifu mkubwa katika eneo la mnara wa kurushia matangazo ya redio huko Bungi.

Mhe. Spika, hali hii inasikitisha sana kwani wananchi wanaofanya uchimbaji huo wa mchanga wanaangalia zaidi maslahi yao binafsi ambayo ni ya muda mfupi ikilinganishwa na umuhimu wa kutunza mazingira ya sehemu hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 56 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imewasiliana na vyombo vya ulinzi na usalama, ili kusaidia kukabiliana na hali hiyo kupitia kwa Mkuu wa Wilaya kwani waharibifu hawa wanafanya uchimbaji huo wakati wa usiku na wakiwa na silaha.

(b) Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imewasiliana na wananchi wanaoishi karibu na eneo hilo na kuwaeleza umuhimu wa mnara huo na athari zake pindipo ukianguka.

(c) Mhe. Spika, niwashukuru na niwapongeze sana wale wananchi ambao wanatupa mashirikiano katika kukabiliana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa sababu wajumbe wanataka kujua umaarufu wa yule mwenzetu aliyetangulia

mbele ya haki. Anaitwa Mohamed Saleh Bajuni, baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, niulize swali.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alikiri kwamba uharibifu huo upo, na waharibifu hao wanafanya uchimbaji huo wakati wa usiku. Sasa kwa kuwa eneo hilo la Mnara wa Bungi halina ukuta.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kujenga ukuta ili kuondoa uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(b) Mhe. Spika, mbali na hali hiyo ya uchimbaji na uharibifu wa mazingira, lakini mnara ule hauko katika mazingira mazuri. Je, wizara ina mpango gani angalau kuutia rangi mnara huo, ili kuwa katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika.

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba sehemu hii inahitaji kujengwa ukuta, lakini nimwambie Mhe. Mwakilishi, kwamba ukiacha ukuta sisi sehemu ile tumeihifadhi kwa kujenga uzio, ili kuhifadhi mnara wetu usipate uharibifu.

(b) Mhe. Spika, pia niendelee kuungana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna haja mnara ule kuwekwa rangi, nikuahidi Mhe. Mjumbe kwamba serikali ikishirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, tutahakikisha kwamba mnara huu tumeuweka rangi na umeleta uhalisia wake mzuri na wa kuridhisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Mhe. Mjumbe uliyekaa baina ya Mhe. Jaku Hashim na Mhe. Suleimani, uliza swali la nyongeza nipe na jina lako.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii. Mimi naitwa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, mimi nilikuwa na swali dogo tu.

Mhe. Naibu Waziri, je, mnara huu wa Bungi umefanyiwa uchunguzi mara ngapi kwa ajili ya usalama wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba mnara huu tunaufanyia uchunguzi kila mara au kila mwaka, kwa ajili ya kuona mazingira ya mnara huu yanakua mazuri, na unakidhi haja na unafanya kazi vizuri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa wizara hii.

Mhe. Spika, redio ni mdomo wa serikali na *ZBC* ina redio Zanzibar ambayo inatakiwa i- *cover* maeneo mengi sana kwa upande ule wa Zanzibar. Lakini cha kusikitisha redio ile haisikikani ipasavyo katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, kulikoni redio Zanzibar usikivu wake umekuwa mdogo kisiwani Pemba, na badala yake redio za FM nyengine zinapata usikivu mkubwa katika kisiwa kile cha Pemba?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nakiri kwamba na ninaungana na yeye Mhe. Mwakilishi kwamba redio yetu ya Zanzibar ina mapungufu wakati mwengine ya kukatika kwa matangazo yake, na wananchi wanakuwa hawafarijiki vizuri na redio yao.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba hii inatokana wakati mwengine na mitambo yetu, au wakati mwengine inasababishwa na umeme. Lakini nimuombe suala hili kwa kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikishirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, tumejipanga hili tatizo tuliondoshe na redio yetu isikike vizuri, ili wananchi wafarijike na redio yao ya Zanzibar bila kutumia redio nyengine za nchi tofauti.

Nam. 100

Tatizo la Udhalilishaji Wanawake na Watoto

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imekumbwa na tatizo kubwa la ubakaji na udhalilishaji wa wanawake na watoto, na kwa kuwa tatizo hili linazidi kuongezeka badala ya kupungua katika jamii yetu.

a) Je, katika kipindi cha mwaka 2015 ni kesi ngapi ambazo zimeripotiwa kwenye dawati la wanawake na watoto za vituo vya Polisi, kati ya hizo ngapi zimemalizika na ngapi zinaendelea.

b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kesi za namna hii kuchukua muda mrefu.

c) Je, Serikali ina mpango gani wa kesi hizi kuona zinamalizika kwa muda mfupi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunipa nafasi tena kusimama mbele yenu kwa ajili ya kujibu swali kama alivyoomba Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, nataka kusema tu kwamba huwenda majibu nitakayotoa yakafanana na majibu niliyotoa jana, kwa kuwa mengi yanajirudia. Lakini naomba nichukue kwa heshima niweze kuyajibu kama alivyouliza.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu imekumbwa na tatizo kubwa la ubakaji na udhalilishaji wa wanawake na watoto, kwa kuwa tatizo hili linazidi kuongezeka badala ya kupungua katika jamii. Ni swali ambalo liliulizwa. Majibu Mhe. Spika, ni kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa takwimu tulizozipata kutoka Dawati la Polisi la Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto kwa kipindi cha Januari hadi Disemba 2015, jumla ya kesi 579 zimeripotiwa kati ya hizo kesi 444 zimepelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, kesi 26 zilifutwa, kesi 95 zimepelekwa Mahakamani na kati ya hizo 7 ziliondoshwa na 7 zilipatiwa hatia.

Kuna sababu nyingi zinazosababisha kesi hizi kuchukua muda mrefu kukamilika. Mojawapo ni kukosekana kwa namna bora ya kuwasilisha ushahidi Mahakamani.

Mhe. Spika, pia katika baadhi ya kesi hizo, watuhumiwa ni watu wa karibu na familia, kutokana na sababu hiyo, kumejengeka tabia ya baadhi ya watu kurubuniwa kwa kutaka suluhu ndani ya familia au kupokea fidia kinyume na matakwa ya Sheria. Polisi na Mkurugenzi wa Mashtaka nao kuchukua muda mrefu kukamilisha uchunguzi.

Mhe. Spika, mfano mdogo tu. Mtoto mwenye umri wa miaka 7 akipelekwa mahali akaulizwa maswali, halafu akaachwa baada ya mwezi mmoja, siku atakayotakiwa ushahidi baada ya mwezi mmoja basi kinachojitokeza ni kwamba yule mtoto hawezi kujibu maswali sahihi kama alivyokuwa amejibu siku ya kwanza, kwa hivyo hilo linakosesha ushahidi.

Hata hivyo, kutokana na hofu ya muathirika kuona hatatendewa haki wakati wa hukumu, anamuomba Hakimu au mwanasheria wake kwamba sina imani na mtu atakayemuhukumu. Kwa hivyo, akishafanya hivyo lile suala inabidi lianze upya tena.

Mhe. Spika, sababu nyengine ni urasimu wa uendeshaji wa kesi hizo ambazo huchukua muda mrefu, hadi mashahidi na waathirika kukata tamaa na kutohudhuria Mahakamani. Kesi inaweza kutajwa kwa miaka miwili bila ya kusikilizwa; tukio ambalo linamfanya muathirika kuamua kuacha kuendelea na kesi.

Mhe. Spika, suala la upendeleo ambapo mara nyingi linaendana na undugu mara nyingi linapelekea kesi hizi kuchukua muda mrefu kuhukumiwa pamoja na kukosekana kwa vifaa vya kuhifadhi na kupatikana kwa ushahidi ikiwemo kipimo cha *DNA*, ambapo kipimo hichi kimechukuliwa kama chaka la kujifichia kwa vyombo vya Sheria, kwamba kwa kuwa hakipo inabidi kisubiriwe kwa muda mrefu na ushahidi unakosekana. Japokuwa serikali kwa makusudi kabisa imejitahidi kuhakikisha kwamba chombo cha *DNA* kinapatikana, na nadhani sasa hivi kipo.

Mhe. Spika, pia suala la watendaji wa sheria wakiwemo Polisi, Mahakama na Waendesha Mashtaka kuwa na mashirikiano madogo katika kuzisimamia kesi hizi, kinapelekea kuzorota mwenendo mzima wa usimamizi wa kesi hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali ina mipango mingi tu ya kuhakikisha kuwa kesi hizi zinamalizika kwa muda mfupi, ikiwemo kuunda Kamati Maalum ya Mawaziri kuhakikisha kuwa kesi hizi zinahukumiwa kwa haraka iwezekanavyo.

Mimi Mwenyewe, kama Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana Wanawake na Watoto, waziri anayesimamia Sheria, waziri anayesimamia elimu na waziri anayesimamia afya. Watendaji wa sheria akiwemo Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi, Mahakimu, Idara ya Ustawi wa Jamii na Vituo vya Mkono kwa Mkono wanaalikwa katika kikao hicho. Kesi mbali mbali zenye matatizo zinajadiliwa katika kikao hicho na kutafutiwa ufumbuzi wake.

Mhe. Spika, aidha Wizara ya Habari, Utalii na Michezo na Wizara ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imeunda Kamati Maalum inayotakiwa kukutana kila robo mwaka kujadili mwenendo wa kesi, ikiwemo kesi ambayo inaitwa *Case Management Committee*. Kamati hii inawajumuisha Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama. Tunaiomba Kamati hii ifanye kazi zake kwa uadilifu kwani bado tunaona kesi hizi hukumu zake zinakuwa hazifikishwi ipasavyo.

Mhe. Spika, wizara inaendelea kutoa mafunzo mbali mbali kwa Mahakimu, Polisi na Waendesha Mashtaka, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Spika, kwa taarifa tu napenda niseme kwamba hivi sasa mapolisi wamekaa katika Hoteli ya *Ocean View* kwa muda wa siku 10, kwa msaada wa watu wanaotoka Uingereza na kiongozi aliyekuwa Polisi mstaafu wa Uingereza, ambaye kwa uzoefu wake tunahitaji uzoefu wake aje atuelimishe na awaelimishe Polisi ni jinsi gani watasaidia ili masuala haya yaweze kumaliziwa hukumu.

Kwa hivyo, kwa msaada wa watu hawa wako pale kwa siku 10 na wanaendelea kwa makini kabisa, waulize kila kitu, wanachukua uzoefu wa kutoka nchi mbali mbali kama Kenya, katika visiwa mbali mbali vile ambavyo vinafanana na sisi.

Mhe. Spika, serikali pia ipo katika hatua ya kuzifanyia marekebisho Sheria zilizopitwa na wakati ikiwemo Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1985 na Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1917.

Mhe. Spika, Wizara imeanzisha namba maalum ya simu (116) kwa ajili ya kupata huduma za haraka na rufaa kwa wahanga wa vitendo hivi. Pia imeanzisha nyumba salama kwa kushirikiana na Shirika la *Action Aid*, ili kuweza kuwasaidia na kuwahifadhi wahanga wakati kesi zao zinaendelea. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kabla sijamuuliza Mhe. Waziri swali langu la nyongeza ambalo litakuwa lina kipengele (a) na (b) naomba Mhe. Waziri afanye marekebisho kidogo, wakati anaanza kujibu swali hili la msingi alisema ni swali lililoulizwa na Mhe. Mussa

Ali Mussa Mwakilishi wa Ole. Lakini aliyeuliza swali ni Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni.

Baada ya marekebisho hayo sasa nije kwenye swali langu la nyongeza ambalo litakuwa na vipengele a) na b) kama ifuatavyo:

a) Ni lini Serikali au Wizara yake itakaa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa ajili ya kuzifanya hizi kesi za udhalilishaji ili ziende haraka zaidi.

b) Kwa kuwa kuna changamoto kubwa katika kesi hizi hasa katika ukaaji wa ushahidi, je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kutoa mafunzo au elimu kwa jamii kuhusiana na kukaa ushahidi wa kesi hizi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza ningeomba niombe radhi kwamba kwenye *quotation* ya kesi yangu ilionesha Mwakilishi aliyetaja samahani sana. Lakini pia nitakalosema tu Wizara yangu kwa makusudi inataka kufanya mpango maalum kwanza niko katika kuhakikisha kuangalia ni kitu gani kitakachokuwezesha kuhakikisha mafunzo yote yanatolewa kwa wananchi kwa njia rahisi.

Kuna kamati mbali mbali ambazo zinafanyika katika shehia mbali mbali za wanawake ambazo zinasaidia katika kuingilia kati na kuhakikisha kwamba masuala yote yanayopelekwa yanahusiana na masuala ya unyanyasaji na jinsia wanawashauri, lakini pia suala zima la kuweza kukaa na hawa wahusika maalum wa mashtaka unafanywa. Na tumeomba kabla hatujakaa nao tuweze kupendekeza baadhi ya sheria, baadhi ya vipengele vitakavyoweza kutusaidia kurahisisha na kutoa zile sheria zilizokuwa zimepitwa na wakati, ili tutakapokuwa tunawashauri tuweze kuona ni jinsi gani itakavyoweza kuwa rahisi.

Lakini nawaombeni kwa mara nyengine kama nyinyi ni wahusika wakuu, tafadhalini tusaidieni kusoma sheria hasa sheria ya udhalilishaji, na wale watakaokuwa na mapendekezo yoyote kwa ajili ya kusaidia Wizara watuletee tuweze kufanya kazi. Waheshimiwa baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimshukuru Waziri kwa majibu mazuri na ya ufasaha kabisa ambayo kajibu lakini na mimi nilikuwa nataka nimuulize swali dogo la nyongeza

Kwa kuwa miongoni mwa watoto waliodhalilishwa wanakuwemo watoto walemavu, na tuna ushahidi wa kesi ya mtoto mlemavu mwenye sura mfanano wa Jimbo la Dimani ambaye alishindwa kujitetea katika kesi yake ya kudhalilishwa, na ikafikia pahala kwamba Idara ya walemavu kesi ile wakaingilia kutokana na Wizara yako kutoweza kufanikisha suala hilo.

Je, Wizara yako sasa hivi ina mikakati gani au mipango gani ya kuweza kutengeneza kitengo cha kuwasaidia watu walemavu ambao wanadhalilishwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Mwakilishi na pia akiwa ni Naibu Waziri wa Elimu au siye, wee.

Mhe. Spika: Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mtanisaidia sana mkitamka majina yenu kabla hamjauliza ili niweze kujibu ipasavyo, kwanza leo mmependeza mmevaa kofia ndio mmenichanganya kabisa.

Mhe. Spika, nasema kwamba suala hili la udhalilishaji linasikitisha sana, ni suala ambalo mimi kwa mara nyingine nasema kwamba wahusika wakuu wanaotushauri kwenye dini, na kama siku ya leo ni siku ya Ijumaa, wachukue hatua kabisa ya kugusa mioyo ya wananchi waweze kuwa na huruma. Kitendo cha kwenda kumdhalilisha mzee hata wewe mtu una akili timamu ni hamu gani inayokufanya hata ukamguse mtu wa namna hiyo. Kwa kweli ni kitu ambacho kinasikitisha sana, lakini ndio pale nilipozungumza kwamba kuna masuala mengine tukichukua sheria peke yake pasipo kuingiza kipengele cha kusema kwamba mazingira yaliyoko yanaweza kuthibitisha kwamba kitendo kile kimefanyika, hatutaweza kufanikiwa katika suala hili, kwa sababu sheria zilizopo zinataka mambo ya ushahidi wa kutizama, sijui kugusa, kufanya nini, ni kitu ambacho nawaombeni sana na nawasihi nyinyi.

Pia suala hilo kwenye kitengo changu kama ni Wizara japokuwa masuala ya Wazee yapo katika ofisi ya Makamu wetu wa Rais, kwa hivyo nitakwenda niangalie nione ni mahali gani tunaweza kukiweka. Ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la mwisho.

Mhe. Waziri katika majibu yako ulilielezea Baraza hili kuwa mtoto wa miaka saba mara nyingi unapokuja kumu- *interview* mara ya pili anapoteza ushahidi wa awali, nimeridhika sana na majibu hayo, lakini naomba sasa utusaidie kwa kuwa Wizara ilishajua kuwa mtoto wa miaka saba ukimuuliza leo baada ya tukio na ukija kumuuliza mara ya pili anapoteza ushahidi wa awali, Wizara tayari imeshajua pana mapungufu.

a) Je, mkakati gani wa Wizara yako mliouweka wa kumsaidia huyu mtoto ili kupata uhalisia wa haki yake ya msingi.

b) Kwa nini mpaka sasa Wizara yako isiandae pale unapomu-*interview* kukawa kuna rekodi maalum itakayowezesha kuendelea na ule uhalisia wa kesi hii na mwenendo wa ushahidi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Kwanza nipate kusema tu kwamba wewe kama mzazi unajua jinsi gani mtoto wa miaka saba au chini anavyokuwa na michezo mingi mno. Michezo yake ya kucheza peke yake anakuwa na rekodi nyingi sana anaziweka kichwani, na mara nyengine akiendelea kuzoza anaingia hofu, lakini kwa makusudi kabisa tunasema ushahidi mwingi unapowekwa unapotezwa.

Wizara yangu itajitahidi sana kuhakikisha kuangalia sehemu zile ambazo zinatunza ushahidi kuwe na *documentation* ambazo ni nzuri pamoja na vifaa vya kisasa, kukiwa na vifaa vya kisasa vikawekwa kwenye *database* sasa hivi kuna *camera*, kuna picha kuna mambo mengi ambayo tukiyashirikisha ili kuwasidia hawa watunza kumbukumbu tunaweza kufanikiwa.

Kwa hivyo nahisi kabisa kwamba ni jambo ambalo hata wanaonisikia wanahusika katika vyombo hivi kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha kwamba tunatunza kumbukumbu hizo, lakini pia kama Wizara ya Wanawake na watoto kwa sababu wengi wanakuja kuripoti kwetu kumbukumbu zinawekwa, ndio maana tunafika pahala pengine tunasema hili jambo lilikuwa hivi lakini anayetoa hukumu ni mwengine sio yule anayepeleka masuala ya ushahidi.

Hilo la pili kama sijalikosea naomba ulirudie tena Mheshimiwa, naomba utaje na jina nikutaje wasikie wananchi wako.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Naitwa Miraji Khamis Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni. Swali la pili kwa kuwa ule uhalisia unapotea kwa nini unapomu-*interview* mara ya mwanzo huyu mtoto, na naamini utaratibu kisheria unaruhusu, kwa sababu hata Mahakama huko mbele tunataka ziende *live*,

unapomu-*interview* huyu mtoto kusiwe na rekodi maalum itakayoweza kutengeneza ile *package* ya kumuhoji na yeye anatoa ushahidi ili kutengeneza uhalisia wa ushahidi wa mwenendo wa kesi inavyokwenda huko mbele.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Nadhani nimekujibu kusema kwamba tutajitahidi sasa hivi kutokana na kutumia vyombo vya kisasa pamoja na kurekodi, pamoja na kuhakikisha mtoto anawekewa kumbukumbu ipasavyo kutia kwenye *database* tuendelee kuwasaidia, na tutajitahidi kushajihisha vyombo vinavyohusika kuhakikisha kwamba wanakuwa na vyombo vya kisasa vitakavyotusaidia kutunza kumbukumbu. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri ameyajibu na hasa kwenye masuala haya ya udhalilishaji na ushahidi, ni vyema kwanza Waheshimiwa Wajumbe wakatambua Sheria ya ushahidi ambayo inaongoza sasa hivi ni ya mwaka 1917, mwakani inatimia umri wa miaka mia moja. Kwa hivyo kuna mambo mengi ambayo yametokea katikati hapa ambayo inabidi sheria ile sasa ifanyiwe mabadiliko, ili haya yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyauliza yaendane na wakati.

Ni kweli sasa hivi mtoto wa miaka saba anayedhalilishwa ili upate ushahidi ni lazima aulizwe yeye yule mtoto atoe ule ushahidi, na wakati mwengine imekuwa vigumu kwa watoto kutoa huo ushahidi.

Sasa kinachofanywa sasa hivi ni kwamba tayari Serikali inaifanyia mapitio ile sheria ya ushahidi, ili sasa hivi vikwazo ambavyo vinatokea viweze kusawazishwa na kesi zile sasa zianze kushughulikiwa kwa haraka na ukamilifu.Nakushukuru Mheshimiwa.

Nam. 45

Malipo ya Fidia kwa Wananchi wa Ole

Mhe. Mussa Ali Mussa – Aliuliza:-
Kwa muda mrefu wananchi wa Jimbo la Ole wamekuwa na kilio kwa Serikali baada ya kusubiri haki yao stahiki na wengine wameshatangulia mbele ya haki wakisubiri malipo ya nyumba zao kwa kupisha ujenzi wa barabara nayokwenda Ole Kianga, Vitongoji, Pujini, Chambani, Kengeja.

a) Je, Serikali inalijua tatizo la wananchi kutokulipwa fidia yao.

b) Je, Serikali itawalipa lini wananchi hao haki yao hiyo huku wengine wakisubiri kwenye vitanda.
c) Je, Serikali inadaiwa kiasi gani na wananchi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inafahamu kilio hicho na ndio maana tayari Wizara imeshafanya tathmini kuanzia Ole/Vitongoji ikijumuisha tathmini ya Nyumba na Vipando na tathmini hizo tunazo.

b) Mhe. Spika Serikali inalipa hatua kwa hatua, sasa hivi Wizara imeshaanza kulipa kwa kuanzia Shehia ya Ole.

c) Mhe. Spika, kiasi ambacho Wizara inadaiwa kutoka Ole hadi Vitongoji ni jumla ya Shs (300,000,000/=).

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifutavyo:
a) Je, Serikali inalijua tatizo la wananchi kutolipwa fidia yao.
b) Je, Serikali itawalipa lini wananchi hao haki yao hiyo huku wengine wakisubiri wakiwa kwenye vitanda.
c) Je, Serikali inadaiwa kiasi gani na wananchi hao.

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa atajibu swali la (a) na (b) tu. Kwa mujibu wa kanuni ni maswali mawili tu, kwa hivyo atajibu la kwanza na la pili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama nilivyomwambia mwanzo kwamba Wizara inajua umuhimu wa kilio chao wananchi na ndio maana ishaanza kulipa fidia awamu kwa awamu, awamu ya mwanzo ililipa milioni 30.6, na awamu hii ya pili akiwemo yeye mmojawapo waliofaidika na hii awamu ya pili tumelipa milioni 60.5. Kwa hivyo Serikali inaendelea kulipa hatua kwa hatua na hali pale inaporuhusu hadi kulipa fidia yote ya milioni mia tatu (300).

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Sambamba na majibu mazuri sana yenye kutia matumaini kwa wananchi wa Zanzibar, suala la kuwalipa fidia wananchi wa Ole, Kianga pamoja na Vitongoji, na mimi naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.
Kwa kuwa ujenzi huu wa barabara wa eneo hili unalingana fika na ule ujenzi wa barabara kuanzia Amani/Dunga, na kwa kuwa katika ujenzi ule wapo watu wengi ambao waliathirika na ujenzi ule na Serikali iliahidi kulipa fidia.

Je, ni lini sasa Serikali itaamua kuwalipa fidia wananchi wa Mwera Mabonde ya Mpunga kama ambavyo waliweza kuwasilisha taarifa yao jumla ya watu nane kwa niaba ya watu wengine ili kuweza kupatiwa fidia hiyo.

Je, ni lini sasa Serikali itarudi na kuweza kuwapa kiasi chao ambacho walikuwa wakikiomba kwa Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama alivyosema mwenyewe kwamba wao wameleta maombi yao, na kama ninavyojua mimi kwamba suala hili lipo la msingi lakini kama anataka nimjibu hapa sasa hivi, basi namwambia tu kwamba Serikali itachukua hatua kuwalipa wahusika hali pale itaporuhusu.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).
Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba tayari Serikali imeshalipa wananchi wa vitongoji vya Ole na Vitongoji kwa kulipa Shilingi milioni 300. Swali langu.

a) Ni wananchi wangapi waliofaidika na malipo hayo ya Shilingi milioni 300.

b) Katika majibu yake pia amesema kwamba wananchi waliolipwa ni Ole/Vitongoji bado wananchi wa Pujini, Chambani na Kengeja, ni lini wananchi hao wa Pujini, Chambani na Kengeja yenyewe watalipwa fidia yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama nilivyosema mwanzo si kwamba tushawalipa milioni mia tatu, bali fidia kutoka Ole hadi Vitongoji wanatudai kwa tathmini yetu na baadae Wizara ya Fedha inakwenda kufanya tathmini zaidi kabla ya kulipa, tunadaiwa milioni mia tatu, lakini mpaka sasa hivi tushalipa milioni 91.1 na awamu ya mwisho tumelipa Mwezi wa Aprili mwaka huu wa fedha.

Suala la pili tunamwambia kama tulivyomwambia mwanzo kwamba hivi sasa tumeanza ujenzi ambao tushafika mpaka *subgrade* na sasa hivi tupo *subbase*, kwa hivyo njia hii tuko mpaka nyuma ya Mfikiwa, tukifika huko pia tutaangalia tathmini tutaifanya na baadae tutajua nani wa kumlipa vipando na nani wa kumlipa nyumba. Kwa hivyo namuomba awe na subra na *inshaalla* Serikali inajali wananchi wake, na itawalipa fidia kwa kadri hali itakavyokuwa inaruhusu.

Mhe. Spika: Maswali yamemalizika Waheshimiwa Wajumbe tumemaliza maswali na bahati nzuri sina tangazo lolote la wageni, lakini nina tangazo tu Waheshimiwa Wajumbe naomba niwatangazie Waheshimiwa Mawaziri kwamba huku nyuma ya ukumbi ukiacha ofisi yangu ile ya *VIP* iliyopo hapo mbele, kuna ofisi kubwa ya *VIP* hapa nyuma chini ya Ofisi ya Spika, kwa hivyo nilikuwa naomba Waheshimiwa Mawaziri mnapokuwa na wageni au wenyewe mnataka kujadiliana masuala mbali mbali basi Spika, anaruhusu kwamba ofisi hiyo mnaweza kuitumia kwa ajili hiyo. (*Makofi*)

Natoa tangazo hili kwa sababu pamekuwa na kawaida sasa ya kuazimwa Afisi ya Naibu Spika kwa ajili hiyo, na inafika wakati anakuwa anakosa kufanya shughuli zake kwa sababu Ofisi yake inatumiwa na Mawaziri, kwa hivyo naruhusu Mawaziri wawe wanatumia chumba cha wageni mashuhuri *VIP* ambacho kipo hapa nyuma chini ya Ofisi ya Spika. Kwa hivyo kitakuwa wazi kwa ajili yao iwapo watakuwa na wageni au munataka kujadiliana mambo baina yenu nyinyi wenyewe kwa wenyewe. Waheshimiwa Mawaziri ahsanteni sana.

UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA BARAZA NA WAJUMBE WA TUME YA BAJETI

Katibu Mezani: Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Tume ya Bajeti.

Mhe. Spika: Ahsante, Waheshimiwa tunaingia kwenye hatua nyengine ya shughuli zetu ili kukamilisha zile nafasi ambazo zilikuwa wazi, kwa hivyo tutakuwa na uchaguzi.

Uchaguzi wa kwanza utakuwa uchaguzi wa kumpata Mwenyekiti ambaye atasaidiana na Spika, pamoja na Naibu Spika, pamoja na Mwenyekiti mmoja ambaye tayari yupo. Kwa mujibu wa kanuni zetu Spika anasaidiwa na Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wawili; Mwenyekiti mmoja mwanamme na Mwenyekiti mmoja mwanamke, sasa bahati nzuri sana tulifanya uchaguzi

tukampata Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa nafasi ya Uenyekiti. Sasa uchaguzi wa leo tumeshampata lakini inabidi tumfanyie uchaguzi mbele ya Baraza kwa ajili ya kumthibitisha Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwa ajili ya nafasi hiyo ya Uenyekiti ili tuweze kusaidiana naye katika uendeshaji wa shughuli za Baraza la Wawakilishi.

Baada ya uchaguzi huo kutakuwa na uchaguzi mwengine ambao tutawapata wajumbe wawili, tumeshawapata lakini tutakuwa tunawathibitisha kwa njia ya kura humu ndani ya Baraza la Wawakilishi ambao wajumbe wenyewe ni Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi.

Kama mtakumbuka kwamba katika uteuzi wa Mhe. Rais wa nafasi za mawaziri tulipata upungufu wa watu wawili katika nafasi ile ambao tulikuwa tumeshawachagua. Kwa hiyo, tutafanya kukamilisha shughuli za uchaguzi unaohusu wajumbe hao wawili, na tuna wagombea wawili pia kwenye nafasi hiyo ambao tutakuwa tunawapigia kura ya ndiyo au hapana. Mhe. Mihayo Juma N'hunga na Mhe. Panya Ali Abdalla.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo naomba sasa nimwite Katibu ili waanze taratibu za uchaguzi wa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi.

Katibu Mezani (Ndg. Khamis Hamad): Mhe. Spika, katika kutimiza matakwa ya Kanuni ya 11 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambayo tunajaza nafasi moja ya Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, jina tulililoletewa kwa nafasi hiyo ni la Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, jina ambalo litapigiwa kura ya siri ya "ndiyo au hapana".

Mhe. Spika, kabla ya hatua hiyo mgombea atapata muda wa kujieleza mbele ya wajumbe kwa muda usiozidi dakika tano, na wajumbe wanaweza kumuuliza maswali yasiyozidi matatu.

Baada ya hatua hiyo Mheshimiwa, kwa kutimiza matakwa ya Kanuni ya 147 na 148 ya Kanuni za Kudumu za Baraza, mtajaza nafasi mbili kama ulivyoeleza za Wajumbe wa Tume ya Bajeti na wajumbe wenyewe ni kama uliowataja Mhe. Mihayo Juma N'hunga na Mhe. Panya Ali Abdalla. Wagombea hawa nao pia watapigiwa kura ya siri ya "ndiyo au hapana" na kabla ya hatua hiyo watapata na wao muda usiozidi wa dakika tano kila mmoja kujieleza mbele ya wajumbe, na wajumbe wakipenda wanaweza kuwauliza maswali yasiyozidi matatu.

Mhe. Spika, zoezi la uchaguzi mara baada ya wajumbe hao wote kujieleza hatua itakayofuata ni ya uchaguzi wa Mwenyekiti ambao tutagawa kura na baada ya wajumbe kupiga kura ya Mwenyekiti tutakusanya na kuingia hatua ya pili ya kupiga kura au ya kugawa kura za uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Bajeti.

Mhe. Spika, mara baada ya zoezi la kukusanya kura tutaingia kwenye zoezi la kuhesabu, ambapo utasitisha kikao kwa muda ambao utatangaza na kupisha zoezi la kuhesabu, na baadae kurudi tena kwa ajili ya kutangaza matokeo.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa.

Mhe. Spika: Ahsante, waheshimiwa kwa heshima kabisa sasa naomba nimwite Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ili aje mbele yenu apate muda wa kujieleza, baadae mutamuuliza maswali ambayo hayazidi matatu na baada ya hapo tutafanya hivyo hivyo kwa waheshimiwa wale ambao wanagombea zile nafasi nyengine, ili tupige kura zote kwa wakati mmoja halafu tutoke tuache watu wanaohusika na mambo ya kuhesabu wakafanye hesabu baadae watatuletea matokeo. Kwa hiyo, naomba nimkaribishe Mhe. Mwanaasha Khamis Mussa aje kwenye *podium.*

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, walioko mbele yako ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wapiga kura katika huu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, jieleze muda usiozidi dakika tano, usipungue dakika *at least* dakika tano, watakuwa na maswali ya kukuuliza yasiyozidi matatu utawajibu, baada ya hapo utawaomba kura. Tafadhali.

Mhe. Mwanaasha Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa leo hii.

Niliyesimama mbele yenu jina langu ni Mwanaasha Khamis Juma ambaye nimegombea nafasi ya Uenyekiti wa Baraza, ni Mwakilishi katika Jimbo la Chukwani. Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima naomba ridhaa zenu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mwanaasha.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba pia niwaite kabisa Mhe. Mihayo Juma N'hunga na Mhe. Panya Ali Abdalla ili nao wajieleze kabisa, ili tutakapofanya zoezi la kupiga kura tuzipige zote kabisa kwa pamoja. Kwa hiyo, naomba nichukue heshima kabisa ya kumkaribisha Mhe. Mihayo Juma N'hunga aje mbele ya waheshimiwa ili aweze kujieleza.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga waliopo mbele yako ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wapiga kura katika nafasi unayogombea ya Ujumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, jieleze muda usiozidi dakika tano na baada ya hapo waheshimiwa watakuuliza maswali yasiyozidi matatu, baadaye utaomba kura. Tafadhali Mheshimiwa.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, ahsante sana. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Wajumbe mbali mbali wa Baraza la Wawakilishi, *assalam alaykum.*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa jina naitwa Mihayo Juma N'hunga, Mwakilishi wa Jimbo la Mwera.

Kama ambavyo inasema Kanuni ya 147, Kifungu (g), kwa heshima na taadhima bila ya kuwa na maneno mengi, naomba sana kura zenu ili niwe Mjumbe katika Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Ahsante sana. (*Makofi*)
Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Maswali?
Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Ahsante, Mhe. Mihayo Juma N'hunga, kwa heshima na taadhima sasa nimkaribishe Mhe. Panya Ali Abdalla ili aje mbele yenu.

Mhe. Panya Ali Abdalla, walioko mbele yako ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wapiga kura katika nafasi uliyogombea ya Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, una dakika tatu au zisizozidi tano ujieleze mbele yao, na kama kutakuwa na maswali yasiyozidi matatu utaulizwa na baada ya hapo utaomba kura.

Mheshimiwa tafadhali karibu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana. Awali ya yote na mimi sina budi kwanza kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana katika chombo chetu hiki kitukufu.

Kwa idhini yako mimi kwa jina naitwa Panya Ali Abdalla nimegombea nafasi hii ya Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Kwa heshima kubwa na taadhima naomba nianze na Makamu wetu wa Pili ambaye ni Kiongozi wetu wa Baraza kuomba ridhaa yake, lakini Waheshimiwa Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri wote naomba ridhaa yao, mwisho naomba *backbenchers* wenzangu wote naomba ridhaa yenu mniwezeshe niwe Mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla, Waheshimiwa Wajumbe maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Maswali?

Wajumbe: Maaruf.

Mhe. Spika: Mhe. Panya Ali Abdalla ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Nashukuru Waheshimiwa Wajumbe, nawatakia Ijumaa Karim. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunaenda kwenye hatua ya upigaji kura, kura zetu kwa mgombea wa mwanzo nafasi ya Uenyekiti ina jina la mheshimiwa pamoja na vyumba viwili, kimoja ni "ndiyo", kimoja ni "hapana". Kwa hiyo, mtu ataweka alama ya vyema kwenye chumba ambacho anaona kinamfaa kwa ajili ya zoezi hili. Moja tu aidha "ndiyo" au "hapana", ukiweka kwenye vyumba vyote viwili kura hiyo itakuwa imeharibika, vile vile ukiitumbukiza kura bila ya kuweka chochote itakuwa imeharibika hiyo kura.

Waheshimiwa Wajumbe, na kwa nafasi ile ya Wajumbe wa Tume ya Bajeti wagombea wetu kama tulivyoona ni wawili; Mhe. Mihayo Juma N'hunga na Mhe. Panya Ali Abdalla na wenyewe kura iko katika utaratibu huo huo kuwa na vyumba vya ndiyo au hapana. Kwa hiyo, mtu ataweka alama ya vyema kwenye kimojawapo tu, aidha cha "ndiyo" au cha "hapana" na si vyenginevyo, sio vyumba vyote viwili au kuiacha kura iwe tupu.

Waheshimiwa kwa zoezi la mwanzo litakuwa ni kura ya Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo kura zitakazogaiwa kwanza zitahusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi.

Baada ya zoezi hilo itafuata sasa kura ya wagombea wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Naomba sasa Katibu tafadhali muanze utaratibu wa kugawa kura.

(Hapa karatasi za kura ziligaiwa kwa Wajumbe kwa ajili ya kupiga kura)

Mhe. Spika: Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika chaguzi hizi Spika hana kura ya asili, Spika ana kura ya uamuzi kama ikitokezea mjumbe amepata idadi sawa ya kura za ndiyo na za hapana. Naomba visanduku sasa vipitishwe ili ziweze kukusanywa kura zilizokwishapigwa na wajumbe.

(Hapa kura zilikusanywa)

Mhe. Spika: Kama kuna mtu ameharibu kura yake na anaomba ibadilishwe ruhusa ipo ya kufanya hivyo. Naomba tukamilishe zoezi la ukusanyaji wa kura.

Naomba kama tumeshamaliza tuanze kugawa kura kwa ajili ya sehemu ya pili ya uchaguzi wetu. Ahsante, sasa naomba tuanze zoezi la ugawaji wa kura kwa ajili ya nafasi ya Wajumbe wa Tume ya Bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe, nilisahau kukupeni *quorum* ya upigaji kura, wajumbe waliomo ndani ni 63, kwa hiyo kura halali zitakuwa ni 63.

(Hapa karatasi za kura ziligaiwa kwa Wajumbe kwa ajili ya kupiga kura)

Mhe. Spika: Naomba kura zianze kukusanywa kwa wale wajumbe ambao wameshapiga.

(Hapa kura zilikusanywa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wagombea kama kuna mgombea anahisi anahitaji kuteua wakala kwa ajili ya kwenda kusimamia kura zake au anaamini meza, ningeomba kuwauliza ili muweze kusaidia kukamilisha hili zoezi.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Spika, naamini meza.

Mhe. Spika: Mhe. Mwanaasha anaamini meza.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, ahsante sana nami naomba nifate busara ya mgombea mwenzangu aliyepita na mimi naamini meza.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mihayo Juma N'hunga.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante na mimi naamini meza.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwashukuru sana waheshimiwa wagombea kwa kuiamini meza.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile kura zimeshapigwa, sasa ningewaomba watendaji wazichukue waende wakazifanyie hesabu. Naomba hayo masanduku ya kura yachukuliwe.

(watendaji waliondoka na kura kwenda kuzihesabu)

Mhe. Spika: Waheshimiwa ili kupisha zoezi la hesabu lifanyike kwa utaratibu naomba kwanza niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mnatangaziwa na Mwenyekiti wa Kamati mkutane baada ya kumalizika kwa shughuli hii ya kupiga kura.

Baada ya hapo naomba nisitishe shughuli za Baraza mpaka saa 5:00 kamili ambapo tutarudi kwa ajili ya kuja kupata matokeo ya uchaguzi ambao tumeufanya hivi punde.

(Saa 4:36 Baraza liliahirishwa kwa muda hadi saa 5:00)

(Saa 5:09 Baraza lilirudia)

MATOKEO YA UCHAGUZI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wote waliohudhuria wakati wa kupiga kura kama nilivyosema awali walikuwa ni 63 na kura zote zilizopigwa zilikuwa ni 63. Matokeo ya kura kwa upande wa Mwenyeki, kura zilizoharibika hakuna hata moja, kura zilizomkubali Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ni 62 na kura iliyomkataa ni kura moja. Kwa matokeo hayo napenda nimtangaze Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kuwa Mwenyekiti wetu mpya wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi).*

Matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi wajumbe wote waliohudhuria walikuwa ni 63, kura zilizopigwa zilikuwa 63, kura zilizomkubali Mhe. Mihayo Juma N'hunga ni kura 62, kura zilizoharibika ni moja na kura iliyomkataa haikuwepo.

Kura zilizomkubali Mhe. Panya Ali Abdalla ni kura 62 na kwake pia kura iliyoharibika ni moja na hapakuwa na kura hata moja iliyomkataa. Kwa hiyo, napenda kuwatangazia Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mihayo Juma N'hunga pamoja na Mhe. Panya Ali Abdalla wanakuwa Wajumbe wetu wapya wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Naomba nichukue nafasi hii basi kuwapa wagombea wetu kila mmoja angalau dakika mbili ili waweze kutoa neno la shukurani na nitaanza kwa Mhe. Mwanasha Khamis Juma (Mwenyekiti) ili aweze kuwashukuru wajumbe.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Spika ahsante, kwanza kabisa na mimi niseme narejea tena kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia niwashukuru wajumbe wote walionipa ridhaa ya kuwa niwe mwenyekiti wa

Baraza hili. Lakini na yule ambaye kura yake moja ilinikataa, nimpongeze sana inawezekana yeye ndiye aliyenikubali kuliko wote.

Jengine pia niwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Chukwani ambao wao wamenichagua kuja katika Baraza hili la Wawakilishi, kwa hiyo na wao nawapongeza na kuwashukuru ili Baraza likaona kuwa mimi nafaa niwe mwenyekiti. Nawapongeza sana popote walipo wananchi wa Jimbo la Chukwani.

Mhe. Spika, pia naomba mashirikiano ya dhati kabisa kutoka kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi niko tayari kupata ushauri, kurekebishwa ninapokosea na pia mashirikiano naomba sana, kwako wewe Spika na ofisi nzima ya Baraza la Wawakilishi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kabisa kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* ambaye ametudiriki sisi na kutujaalia kufanikisha zoezi hili katika hali ya uzima na umakini wa hali ya juu.

Pili, nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ambao wametumia haki yao ya msingi na ya kidemokrasia kwa kunipa kura nyingi na kunipa ridhaa ya kuwatumikia ndani ya Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Sambamba na hilo naomba nitumie fursa ya pekee kuwashukuru sana jamii ya wananchi wa Jimbo la Mwera kwa heshima kubwa walionipa na dhamana walioniamini nami nasema sitowaangusha.

Mwisho nimalizie kuishukuru familia yangu ambayo imekuwa ikifanya jitihada kubwa ya kunishauri, kunielekeza na kuniambia baadhi ya mambo mengi ambayo yatakuwa na manufaa ya kujenga na kulisogeza mbele taifa letu.

Mwisho kabisa nasema tunachokifanya tunafanya kwa mujibu wa umoja wetu na mshikamano wetu. Hivyo, kwa umoja wetu natumai tutapata mashirikiano bora kabisa pale ambapo mtahisi tunakwenda sivyo nitakuwa tayari na niko tayari kupata maelekezo kwa dhamira ya kuleta ufanisi mzuri na bora katika majukumu yetu kwa kipindi hiki. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* kwa rehema zake na utukufu wake ambao ametujaalia. Pia na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru wajumbe wenzangu wote wakiwemo viongozi wetu Makamu wa Pili wa Rais, Mawaziri, Manaibu Waziri na Wajumbe wenzangu wote wa Baraza hili kwa imani yao

kubwa waliyoionesha kwangu nasema napongeza na ninaheshimu sana heshima hii ambayo wamenipatia, nami naahidi kwamba heshima hii nitaitunza na nitaithamini na naomba kabisa niendelee kuwaomba wajumbe wenzangu kwamba hii ni kazi na ili kazi iende vizuri basi inahitaji mashirikiano makubwa. Inawezekana wenzetu wakawa wana jambo zuri la kutupa linalohusiana na kazi hii kwa hiyo tuko tayari kulipokea kwa maslahi ya kuendesha chombo chetu hiki lakini pia kwa maslahi ya taifa letu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukue fursa hii pia na mimi niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao ndio waliosababisha kunileta katiba Baraza hili, nawashukuru na nawapongeza sana *Inshaallah* na mimi naahidi sitowaangusha nitajitahidi kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha ili niweze kuwatumikia vizuri.

Mhe. Spika, nami nisiwe mwizi wa fadhila kwa kuishukuru familia yangu, napenda niishukuru familia yangu kwa kunipa mashirikiano makubwa tangu kuanza harakati za uchaguzi mpaka hapa tulipofikia. Lakini pia nimshukuru mume wangu mpenzi Pembe Juma Khamis ambaye kwa hekima na busara kubwa aliyoniamini na kuniwezesha kunipa fursa ya kuweza kufika katika chombo hiki, nami naamini nitalinda heshima hiyo ambayo amenipatia na nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuheshimu sana. Kwa kuwa nina sababu kubwa moja ya kuwa bwana huyu alikuwa ni kiongozi na ni kiongozi mstaafu nitaendelea kugema hekima na busara ambazo alikuwa akizitumia ziniwezeshe kuendeleza majukumu haya kwa faida yangu na wanawake wenzangu lakini na kwa faida ya taifa kwa ujumla. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla nami nikupongezeni nyote kwa pamoja mlioshiriki uchaguzi na kumaliza. Katibu kwa shughuli inayoendelea tafadhali.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja iliyopo mbele yetu ni ya kumtaka sasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje awasilishe hotuba yake ya bajeti, lakini muda nilionao ningemuomba sasa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anipe maelekezo kidogo. Mhe. Waziri wa Nchi tafadhali.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kuwasilisha hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na kwa kuwa leo ni siku ya Ijumaa na wengi wetu hapa ni waumini ambao tunahitaji kwenda kutekeleza ibada hiyo, kwa hivyo Mhe. Spika,

nawaomba wajumbe wako tuweke kando kanuni ya muda ili tuakhirishe Baraza hili mpaka saa 11:00 jioni barabara ili tuweze kuendelea na shughuli zetu na hapo tuweze kuwasilisha hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa hoja imetolewa na naona imeungwa mkono. Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niwahoji kwa wale ambao wanadhani kwamba tuweke kando kanuni ya muda ili kumuwezesha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuja kutoa hotuba yake ya bajeti saa 11:00 za jioni kwa sababu muda tulioao hautoshi, wale wote ambao wanaunga mkono hoja naomba wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nasitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00 za jioni.

(Saa 5:21 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Mtumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee na lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kuweza kutukutanisha hapa leo kwa ajili ya kuipokea hotuba hii, kuijadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ili tupate nyenzo za kutuwezesha kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, namshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake anazozichukua katika kuiongoza nchi yetu. Mhe. Rais amekuwa akitoa maelekezo na miongozo inayotekelezeka na yenye muelekeo wa kutuletea maendeleo na tija katika nchi yetu. Hotuba aliyoitoa wakati akilizindua Baraza la Tisa (9) la Wawakilishi imeonesha wazi azma yake ya kuwahudumia wananchi na kuwaletea maendeleo katika nyanja zote. Ni imani yangu kwamba wananchi wote tutaendelea kumuunga mkono Mhe. Rais katika juhudi zake hizi.

Mhe. Spika, aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi kifupi cha uongozi wake chini ya kauli mbiu ya "**Hapa Kazi Tu"**. Pia nawapongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais Magufuli katika kufanikisha majukumu yake.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa kuliongoza vyema Baraza hili Tukufu. Aidha, nawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza kwa kuteuliwa na kuanza vyema kazi za kusimamia utendaji wa Taasisi za Serikali. Vile vile, natoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Konde, Makamu Mwenyekiti, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mwakilishi wa Viti Maalum na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2016/2017 na kutupatia ushauri na miongozo juu ya Makadirio hayo na kuikubali iwasilishwe katika kikao chako hichi kitukufu.

HALI YA SIASA

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliendesha Uchaguzi Mkuu wa marudio tarehe 20 Machi 2016. Jumla ya Vyama 14 vilishiriki kugombea nafasi ya Urais ambapo Chama Cha Mapinduzi kiliibuka na ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika kipindi cha uchaguzi kulijitokeza hali ya uvunjifu wa amani kwa baadhi ya wananchi kuchoma moto mali za Serikali na za wananchi wenzao vikiwemo vituo vya afya, mashamba ya mikarafuu na nyumba za makaazi. Aidha, kumejitokeza tabia kwa baadhi ya wananchi kususiana na

kubaguana kutokana na tofauti za itikadi za kisiasa katika shughuli mbali mbali za kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha hali ya umoja, amani na utulivu inaendelea nchini. Nachukua fursa hii kutambua mchango mkubwa wa vyombo vya Ulinzi na Usalama katika kusimamia amani ya nchi yetu. Nawaomba wananchi waendelee kushirikiana katika shughuli zao za kijamii pamoja na kutoa ushirikiano kwa viongozi wa ngazi zote za serikali katika kudumisha hali ya umoja, amani na utulivu.

HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 katika Baraza lako Tukufu, uchumi wa Zanzibar umekua kwa asilimia 6.6 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.0 kwa nchi zinazoendelea na asilimia 3.4 kwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, kasi hiyo inaashiria kupungua kidogo ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2014.

Mhe. Spika, pato halisi la Taifa kwa mwaka 2015 limeongezeka na kufikia thamani ya Shilingi 2,308.0 Bilioni ikilinganishwa na thamani ya Shilingi 2,133.5 Bilioni mwaka 2014. Vile vile, wastani wa pato la mtu binafsi limeongezeka kufikia Shilingi 1,632,000 sawa na Dola za Kimarekani 817 mwaka 2015 kutoka Shilingi 1,552,000 sawa na Dola za Kimarekani 939 mwaka 2014 kwa bei za miaka husika. Kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani kwa wastani wa asilimia 20.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2014 imepelekea thamani ya pato la Mtu binafsi kwa Dola kupungua. Hata hivyo, kwa kutumia bei za kudumu za mwaka 2007 bado wastani wa pato la mtu binafsi limeongezeka kutoka Dola za Marekani 651 mwaka 2014 hadi Dola 674 mwaka 2015.

Mhe. Spika**,** kasi ya mfumko wa bei imefikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2015 kutoka asilimia 5.6 mwaka 2014. Kasi ya mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula umeongezeka kufikia asilimia 7.4 mwaka 2015 kutoka asilimia 4.4 mwaka 2014. Aidha, mfumko wa bei kwa bidhaa, zisizo za chakula ulishuka hadi kufikia asilimia 4.0 mwaka 2015 kutoka asilimia 6.8 mwaka 2014. Hali hii inatokana na kushuka kwa bei za bidhaa za mafuta ikiwemo dizeli, petroli na mafuta ya taa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 maeneo muhimu yatakayoendelea kupewa kipaumbele na Serikali ni pamoja na kuhakikisha mapato ya Serikali yanakusanywa kikamilifu, kusimamia utunzaji na uendelezaji wa miundombinu na mawasiliano, kuendeleza utalii, kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuimarisha huduma za elimu, afya, pamoja na maslahi ya wazee nchini.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mafuta na Gesi, Serikali imekamilisha utayarishaji wa Rasimu ya Sera na Rasimu ya Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ambazo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kukamilika kwa sera na sheria hizo kutaiwezesha serikali kuwa na miongozo mizuri katika kusimamia masuala ya Mafuta na Gesi Asilia hapa nchini.

Mhe. Spika**,** katika kuhakikisha wananchi wa vijijini wanapata huduma za umeme, Serikali imejenga njia za kupitishia umeme mkubwa zipatazo kilomita 33.1 na kilomita 83.9 za laini ndogo. Aidha, Serikali imeweka transfoma 35 za kusambaza umeme katika vijiji 36 Unguja vijiji 16 na Pemba 20.

Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda inaendelea kuimarika na tunategemea itachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wananchi. Kuanza kazi kwa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kunatoa matumaini ya kujitegemea kwa sukari hapo baadae. Pia Kiwanda cha Upigaji Chapa, Kiwanda cha Maziwa Fumba, viwanda vya maji na viwanda vyengine mbali mbali vikiwemo vya uchongaji na usindikaji vinatoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa uchumi wetu.

HUDUMA ZA JAMII

Mhe. Spika, huduma za jamii zitaendelea kupewa msukumo mkubwa katika kipindi hiki cha pili cha Awamu ya Saba. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma za elimu, afya, maji safi na salama pamoja na makaazi ili kuleta ustawi mzuri kwa jamii.

Mhe. Spika, sekta ya elimu ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sekta hii ina jukumu la kutoa elimu kwa wananchi wa Zanzibar kwa mujibu wa malengo yaliyoainishwa katika Mipango na Sera ya Elimu, Dira ya Maendeleo 2020 na MKUZA. Katika kufikia malengo hayo, Serikali itaendelea kuimarisha Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari, Elimu Mbadala pamoja na Elimu ya Juu.

Mhe. Spika, Serikali inaendelea kutekeleza programu mbali mbali za elimu ikiwemo programu za vituo vya Tucheze Tujifunze "TuTu" na kufanya tathmini ya vituo hivyo pamoja na kusaidia watoto wenye mahitaji maalum kwa kuwapatia vifaa. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo viwili (2) vya mafunzo ya Amali Makunduchi kwa Unguja na Daya kwa Pemba; Upanuzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia; Upanuzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii pamoja na Kukamilisha Kituo cha Elimu Mbadala – Wingwi Mtemani ili kuwajenga vijana kitaaluma na kiujuzi ili waweze kuingia katika soko la ajira kwa uhakika.

HUDUMA ZA JAMII

Mhe. Spika, huduma za jamii zitaendelea kupewa msukumo mkubwa katika kipindi hiki cha pili cha Awamu ya Saba. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma za elimu, afya, maji safi na salama pamoja na makaazi ili kuleta ustawi mzuri kwa jamii.

Mhe. Spika, sekta ya elimu ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sekta hii ina jukumu la kutoa elimu kwa wananchi wa Zanzibar kwa mujibu wa malengo yaliyoainishwa katika Mipango na Sera ya Elimu, Dira ya Maendeleo 2020 na MKUZA. Katika kufikia malengo hayo, Serikali itaendelea kuimarisha Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari, Elimu Mbadala pamoja na Elimu ya Juu.

Mhe. Spika, Serikali inaendelea kutekeleza programu mbali mbali za elimu ikiwemo programu za vituo vya Tucheze Tujifunze "TuTu" na kufanya tathmini ya vituo hivyo pamoja na kusaidia watoto wenye mahitaji maalum kwa kuwapatia vifaa. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo viwili (2) vya mafunzo ya Amali Makunduchi kwa Unguja na Daya kwa Pemba; Upanuzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia; Upanuzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii pamoja na Kukamilisha Kituo cha Elimu Mbadala – Wingwi Mtemani ili kuwajenga vijana kitaaluma na kiujuzi ili waweze kuingia katika soko la ajira kwa uhakika.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za afya kwa wananchi kwa kuifanya Hospitali ya Mnazimmoja kuwa ya Rufaa kwa kuiongezea huduma za matibabu ya saratani, kuimarisha huduma za uchunguzi *Magnetic Resonance Imaging - MRI*. Hospitali za Abdalla Mzee na Wete Pemba pia zimeendelea kuimarishwa ili zifikie hadhi ya kuwa Hospitali za Mkoa.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na Washirika mbali mbali wa Maendeleo katika utekelezaji wa Miradi/Programu za Afya ikiwemo; Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya, Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Malaria, Mradi Shirikishi wa UKIMWI na Kifua Kikuu, Programu Shirikishi ya Huduma za Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto na Mradi wa Taaluma za Afya. Ni matumaini yangu kuwa shughuli zote hizi zilizopangwa zitatekelezwa kwa ufanisi na kwa maslahi ya wananchi wote.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Uwezeshaji, Serikali inaendelea kukabiliana na changamoto za ajira kwa kuwajengea uwezo vijana ili waweze kujiajiri na kuajirika. Aidha, kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Serikali inaendelea kusimamia jukumu la kutoa mitaji kwa wananchi wenye kipato kidogo ili watumie katika shughuli za uzalishaji mali kwa kujiajiri na kupunguza umasikini. Mfuko huo umefanikiwa kutoa jumla ya mikopo 307 yenye thamani ya Shilingi Milioni 467,278,000. Mikopo hiyo imeelekezwa katika shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, kazi za mikono, usindikaji matunda, viwanda vidogo vidogo vya mafuta ya nazi na mafuta ya mgando pamoja na viwanda vya sabuni za kufulia na kukogea.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa Sekta ya Ujenzi, Serikali inaendelea na ujenzi na matengenezo ya barabara mbali mbali za Unguja na Pemba ili kuimarisha huduma za usafiri kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Katika kipindi cha 2015/2016 miongoni mwa Barabara zinazoendelea na ujenzi ni pamoja na Ole - Kengeja yenye urefu wa kilomita 35, Jendele – Cheju - Kaebona yenye urefu wa kilomita 11.6 na Koani - Jumbi yenye urefu wa kilomita 6.4. Aidha, matengenezo makubwa ya barabara yamefanyika kwa barabara kuu na za ndani.

Mhe. Spika, kwa upande wa uimarishaji wa usafiri wa anga, Serikali inaendelea na kazi ya ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na kazi hiyo inategemewa kukamilika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

MASUALA MTAMBUKA

Mazingira

Mhe. Spika, utunzaji wa mazingira ni suala la lazima na ni muhimu kulitekeleza ili kuleta maendeleo endelevu na kupunguza umasikini nchini kwetu. Nchi zote duniani na mashirika mbali mbali ya kimataifa yanatoa kipaumbele katika suala la kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ili

kupunguza athari zinazotokana na hali hiyo. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikihimiza wananchi kutunza maeneo ya misitu na kupanda miti kwa wingi maeneo ya wazi ikiwemo fukwe za bahari pamoja na kuachana na tabia ya kukata miti ovyo na uchimbaji wa rasilimali zisizorejesheka.

Athari za mvua za Masika

Mhe. Spika, siku ya tarehe 17 Aprili, 2016 ilinyesha mvua kubwa iliyofikia milimita 212.4 na kusababisha mafuriko katika maeneo mengi hasa ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Kufuatia mvua hiyo, jumla ya nyumba 3,330 zenye kaya 4,712 ziliathirika na kuilazimu Serikali kufungua kambi maalum katika Skuli ya Mwanakwerekwe C ili kuwahudumia wananchi hao. Jumla ya watu 420 walihifadhiwa na kupatiwa huduma mbali mbali za kibinaadamu katika kambi hiyo. Athari nyengine zilizotokana na mvua hizo ni upotevu wa maisha ya mtu mmoja pamoja na kupotea kwa mali za wananchi. Nachukua fursa hii kuwapa pole wale wote waliopata athari ya mvua hizi. Naomba kuwanasihi wananchi wenzangu tuache kujenga katika maeneo ya mabondeni na katika njia za maji. Aidha, naziagiza Mamlaka zinazohusika na utoaji wa viwanja na vibali vya ujenzi wafuate taratibu zilizowekwa ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza.

Kipindupindu

Mhe. Spika, mwanzoni mwa mwezi wa Septemba 2015, visiwa vyetu vya Zanzibar vilikabiliwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa maradhi ya kuharisha na kutapika yaliyoripotiwa katika Vituo vya Afya vilivyopo Unguja na Pemba. Baada ya kupata matokeo ya uchunguzi wa kimaabara, ilithibitika kuwepo kwa mripuko wa maradhi ya kipindupindu. Kufuatia mripuko huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, imeendelea kuchukua jitihada za dhati katika kukabiliana na maradhi haya.

Mhe. Spika, Serikali ilifungua kambi maalum za matibabu ya kipindupindu Unguja na Pemba, ambapo hadi kufikia tarehe 11 Mei, 2016 jumla ya wagonjwa 3,897 walilazwa na kutibiwa. Kati ya hao, wagonjwa 2,450 walilazwa katika kambi za Unguja na wagonjwa 1,447 walilazwa katika kambi za Pemba. Jumla ya wagonjwa 59 wameripotiwa kufariki (46 Unguja na 13 Pemba).

Mhe. Spika, mripuko wa maradhi haya katika kipindi hiki, umechukua muda mrefu zaidi kuliko miaka ya nyuma. Sababu kubwa zilizopelekea hali hiyo ni

wananchi kutofuata kanuni za afya na usafi wa mazingira. Hata hivyo, ni jambo linalotia matumaini kuona kwamba maradhi haya tumeanza kuyadhibiti baada ya kuchua hatua mbali mbali. Nawaomba wananchi tuongeze juhudi za kusafisha mazingira yetu pamoja na kufuata miongozo na kanuni za afya. Aidha, nachukua fursa hii, kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati watendaji wote ambao kwa namna moja ama nyengine wanashiriki katika hatua za kulitokomeza janga hili.

Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu ikiwemo ubakaji, kupigwa, kutelekezwa, kuitwa majina mabaya na kunajisiwa ni kubwa katika jamii yetu. Serikali inaendelea na juhudi za kudhibiti vitendo hivi vya udhalilishaji na itaendelea kuchukua hatua kwa wale wote watakaojihusisha na vitendo hivyo. Kwa mantiki hiyo, naviagiza vyombo vya kusimamia haki na sheria kutimiza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kuzishughulikia kesi za namna hii kwa haraka na kuwapatia haki watu wenye ulemavu ili kulinda utu wao**.** Pia, naiasa jamii kuacha vitendo vya udhalilishaji kwa Watu Wenye Ulemavu kwani wao pia ni binaadamu na wanastahiki kuheshimiwa na kutendewa haki na kupatiwa fursa sawa katika jamii.

Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa

Mhe. Spika, wakati wa kulizindua Baraza lako hili Tukufu tarehe 05 Aprili, 2016 Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alilikemea kwa nguvu zake zote suala la rushwa na kusisitiza masuala ya uwajibikaji na utawala bora. Katika kufikia azma hiyo Serikali inaendelea kutekeleza Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Namba 1 ya mwaka 2012 pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 4 ya mwaka 2015. Hatua za utekelezaji wa Sheria hizi unaendelea ambapo hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amemteuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kusimamia Maadili ya Viongozi ili Tume hiyo iweze kuanza kazi rasmi.

Hali ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI

Mhe. Spika, kiwango cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI hapa Zanzibar ni asilimia 1 na kuwa ni miongoni mwa nchi chache kusini mwa Jangwa la Sahara yenye kiwango cha chini cha maambukizi ya UKIMWI. Maambukizi haya yanawaathiri zaidi wanawake kuliko wanaume kwa uwiano wa 3 kwa 1. Hata hivyo, kuna makundi maalum ambayo kiwango cha maambukizi ni

kikubwa ukilinganisha na kile kilichomo katika jamii. Makundi hayo ni wanawake wanaojiuza (19.3), wanaojidunga dawa za kulevya (11.3) na wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao (2.9). Serikali itaendelea na jitihada za kupambana na ongezeko la maambukizi kwa makundi yote haya na jamii kwa jumla. Natoa wito kwa wananchi kuendelea kubadili tabia na kudhibiti mazingira hatarishi kwa maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kuacha kuwanyanyapaa watu wenye maambukizo ya Virusi vya UKIMWI.

Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, Dawa za Kulevya bado ni tatizo sugu duniani kote na hapa Zanzibar linaendelea kutuathiri siku hadi siku. Hali halisi inaonesha kwamba vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa ndio wanaoathirika zaidi na matumizi ya dawa hizo. Katika kupambana na changamoto hii Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuchukua hatua za kuondoa kabisa usafirishaji na usambazaji, matumizi na athari zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Hivyo, nachukua fursa hii, kuvitaka vyombo vyote vinavyosimamia udhibiti wa dawa za kulevya kufanya kazi hiyo kwa uadilifu mkubwa ili kurahisisha utekelezaji wa mipango ya udhibiti wa dawa hizo.

MALENGO NA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI-MACHI) 2015/2016

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) cha mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake imechukua juhudi kubwa katika kutekeleza malengo iliyojipangia katika Programu zake kama ifuatavyo:-

1. ***Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais (C011)***

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i) Ofisi imeratibu ziara 16 za ndani ya nchi pamoja na kutekeleza ahadi 10 za masuala mbali mbali zilizoahidiwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais;

ii) Ili kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa nchi na Taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, Kikanda na Kimataifa, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikutana na Wageni Mashuhuri na Mabalozi wa nchi 14;

iii) Ofisi imefanya matengenezo makubwa katika nyumba ya makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mazizini na Dar es Salaam na;

iv) Ofisi imempatia mafunzo ya muda mrefu mfanyakazi mmoja nje ya nchi. Aidha imewalipa stahiki za likizo wafanyakazi watano (5).

2. **Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali (CO12)**

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Ofisi imetayarisha Taarifa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 - 2015 kwa kipindi cha miaka mitano (Novemba, 2010 hadi Julai, 2015);

ii. Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, ikiwa ni pamoja na kufuatilia marejesho ya matumizi ya fedha za mwaka 2014/2015 pamoja na kufuatilia miradi iliyotekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko huo. Pia, Ofisi imeandaa Rasimu ya Kanuni ya Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ambayo inatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka wa fedha wa 2016/2017;

iii. Ofisi imeratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini *(TASAF III)* unaotekelezwa katika Shehia 204 (Unguja 126 na Pemba 78). Katika kipindi cha miezi tisa, Ofisi imefanya malipo kwa Kaya Masikini 33,632 (Unguja 18,944 na Pemba 14,688) ambapo jumla ya Shilingi 6,188,276,000 zimelipwa. Aidha, mafunzo ya wataalamu 20 wa kisekta kuhusu uibuaji na usanifu wa miradi 94 ya kutoa ajira za muda (Unguja 43 na Pemba 51) yamefanyika. Mafunzo juu ya kujaza fomu za masharti ya elimu na afya yametolewa kwa watumishi wa vituo vya afya na walimu 338 (Unguja 135 na Pemba 203) wa skuli zinazohusika na Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa Unguja na Pemba;

iv. Ofisi imeandaa muundo mpya na kutayarisha mapendekezo ya uendeshaji wa Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam;

v. Ofisi imetoa mafunzo ya kujiandaa na kukabiliana na maafa kwa wanafunzi wa skuli za Msingi na Sekondari kwa Wilaya za Kusini, Kati na Kaskazini ‘B’ kwa Unguja, Mkoani na Chake Chake kwa Pemba ambapo jumla ya wanafunzi 500 wa Skuli za Msingi na 490 wa Sekondari wamepatiwa mafunzo hayo;

vi. Ofisi imeratibu na kutoa huduma katika majanga na maafa yaliyotokea ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba yakiwemo maafa ya mafuriko, ajali za moto na maradhi ya kipindupindu;

vii. Ofisi imeendesha mafunzo kwa wafanyakazi 22 wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, watano (5) kutoka Wilaya tano za Unguja na Pemba na mmoja kutoka *ZBC radio* walishiriki katika ziara ya kimafunzo ya wiki moja juu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa katika Wilaya za Kinondoni, Kilosa na Chamwino Tanzania Bara. Aidha, makongamano matatu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa yameendeshwa kwa wanafunzi kutoka Chuo cha Utawala wa Umma (*IPA*) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*ZIFA*) kwa upande wa Unguja pamoja na Chuo cha Ualimu Benjamin Mkapa kwa upande wa Pemba;

viii. Ofisi imeratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na kusimamia kilele cha Sherehe hizo zilizofanyika tarehe 12 Januari, 2016 Uwanja wa Amaan;

ix. Ofisi imeratibu Hitima na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume iliyofanyika Afisi Kuu ya CCM, Kisiwandui tarehe 7 Aprili, 2016 na;

x. Ofisi imejenga kaburi la Rais Mstaafu wa Zanzibar wa Awamu ya Nne, Marehemu Sheikh Idris Abdulwakil huko Makunduchi na kuendelea kusimamia mazingira ya eneo lilipo kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, Kisiwandui.

Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa (C013)

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Ofisi imetayarisha Rasimu ya Sheria inayoipa mamlaka Kiwanda cha Upigaji chapa iwe Taasisi inayojitegemea;

ii. Ofisi imechapisha nyaraka na machapisho mbali mbali ya Serikali kama vile Gazeti Rasmi la Serikali, Miswaada ya Sheria, Sheria na machapisho mengine yaliyowasilishwa kiwandani kwa mujibu wa mahitaji ya Taasisi husika na;

iii. Ofisi imenunua mitambo mipya kwa awamu ya pili ambayo tayari imeshaanza kufungwa kiwandani.

4. ***Programu ya Mipango na Utawala (C014)***

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi imefanikiwa kununua vifaa mbali mbali vya kuendeshea kazi ikiwa ni pamoja na kompyuta tatu (3); Aidha, Ofisi imelipia huduma za maji, umeme, mawasiliano pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi;

ii. Ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 28, wafanyakazi 27 wapya wamepatiwa mafunzo ya awali *(Induction Course)* pamoja na kulipia stahiki za likizo kwa wafanyakazi 72;

iii. Ofisi imefanya kikao kimoja cha Kamati ya Uongozi, vikao vitatu vya Kamati ya Ukaguzi na kikao kimoja cha kujadili makisio ya mishahara na maposho ya wafanyakazi. Aidha, Ofisi imeratibu na kusimamia vikao vitatu vya Bodi ya Zabuni na kuendelea kulifanyia mapitio daftari la mali za Serikali;

iv. Ofisi inaendelea na utayarishaji wa ripoti ya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ili kuandaa mpango mkuu wa mafunzo;

v. Ofisi imeandaa Taarifa za Utekelezaji kwa kipindi cha mwaka mzima 2015/2016, miezi sita (6) Julai - Disemba na taarifa ya Utekelezaji miezi mitatu (Oktoba – Disemba) 2015/216. Aidha, Ofisi imetayarisha Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na;

vi. Ofisi kwa kupitia kitengo cha Kusimamia miradi ya Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Kupambana na maradhi hayo (*ZGFCCM*) imeendesha vikao viwili vya robo mwaka vya kawaida na Kikao kimoja cha dharura pamoja na vikao vyengine vya Kamati vikiwemo Kamati ya *"Oversight ommittee",* Kamati Tendaji na Kamati ya Fedha. Aidha, Kitengo kimefanya uchaguzi wa kuwapata wajumbe wake katika majimbo saba ya *ZGFCCM* ambayo yanaundwa na Sekta tofauti.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Programu ya 1: ***Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali (CO21)***

Programu ya 2: ***Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi (CO22)***

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza la Wawakilishi limetekeleza yafuatayo:-

i. Ofisi kupitia Baraza la Wawakilishi limekamilisha mkutano wa ishirini ambao ulikuwa ni wa mwisho kwa Baraza la Nane (2010 – 2015);

ii. Ofisi kupitia Baraza la Wawakilishi ilisimamia uzinduzi wa Baraza jipya la Tisa;

iii. Mafunzo elekezi juu ya majukumu ya Mjumbe wa Baraza la tisa (9) yalitolewa na;

iv. Ofisi imewapatia mafunzo watumishi 17 katika ngazi na fani mbali mbali, kama vile Sheria, Utawala. Utawala wa Fedha, Utawala wa rasilimali Watu. Ukatibu Muktasi, Ukutubi, na Ukarani masjala kwenye ngazi ya Digrii ya Kwanza, Digirii ya Juu na Digrii ya Uzamivu.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Programu ya 1: Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi

Programu ya 2: Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Tume ya Uchaguzi imetekeleza yafuatayo:-

i. Ofisi kupitia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeendesha na kusimamia Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Madiwani;

ii. Ofisi imesomesha wafanyakazi wawili kwa kiwango cha Shahada ya Pili na Shahada ya Kwanza kwa lengo la kuongeza taaluma na kuleta ufanisi zaidi katika utendaji wa kazi. Aidha, wafanyakazi watatu walipatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini Afrika ya Kusini yanayohusiana na mambo ya Uchaguzi;

iii. Ofisi iliandaa Semina kwa Majaji na Mahakimu kwa lengo la kutatua migogoro na kesi za uchaguzi;

iv. Ofisi imeendesha makongamano kwa vijana ili wapate uelewa zaidi kuhusiana na Uchaguzi, kwa lengo la kuwaepusha kujiingiza katika vurugu;

v. Ofisi kupitia Tume ya Uchaguzi kwa kushirikikiana na *UNDP* iliandaa Semina kwa Vyama vya Siasa, vilivyoshiriki katika Uchaguz;

vi. Ofisi kupitia Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na *UNDP* imetoa elimu ya Mpiga Kura katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa lengo la kuwawezesha wapiga kura kupata uelewa mzuri wa Uchaguzi na;

vii. Ofisi imenunua vifaa vya kuweka kumbukumbu za wapiga kura zikiwemo sava, kompyuta na printa za kuchapisha kadi pamoja na kulipia huduma za mitandao.

UTEKELEZAJI KIFEDHA KWA PROGRAMU

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 625,568,698 kwa ajili ya Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya Shilingi 357,646,714 zilipatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 57.2 Kiambatisho Nam. 1

Mhe. Spika, katika mwaka 2015/2016 Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 2,239,727,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2016, Programu hii imeingiziwa jumla ya Shilingi 1,397,031,987 ikiwa ni sawa na asilimia 62. Kiambatisho Nam. 1.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 714,050,000 kwa Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya Shilingi 479,710,617 zimetumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 67. Kiambatisho Nam. 1.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 1,587,354,000 kwa Programu ya Mipango na Utawala. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya Shilingi 949,727,773 zimetumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 60. Kiambatisho Nam. 1.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 16,762,600,000 kwa programu za Baraza la Wawakilishi. Hadi kufikia Machi 2015 jumla ya shilingi jumla ya Shilingi. 4,546,691,512 zimetumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 27**.** Kiambatisho Nam. 1.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 1,404,000,000 kwa programu za Tume ya Uchaguzi. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Shilingi 885,251,255 zimetumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 63**.** Kiambatisho Nam. 1

UKUSANYAJI WA MAPATO

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inakusanya mapato kutoka Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika kipindi cha Miezi Tisa (Julai - Machi 2015/2016), Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 600,000,000. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2016 Ofisi imekusanya jumla ya Shilingi 279,145,120 sawa na asilimia 47 ya lengo. Aidha, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 12,360,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2016, Ofisi imekusanya Shilingi 10,180,000 sawa na asilimia 82 Kiambatisho Nam.2.

UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZILIZOHAMISHIWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, kufuatia mabadiliko ya Muundo wa Serikali yaliyofanyika katika Serikali ya Awamu ya Saba kipindi cha Pili, Idara moja (1) na taasisi mbili (2) zilizokuwa chini ya iliyokuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais zimehamishiwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Taasisi hizo ni:-

i. Idara ya Watu Wenye Ulemavu;
ii. Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti na Uratibu wa Dawa za Kulevya na;
iii. Tume ya UKIMWI

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Spika, kazi za Programu hii zimetekelezwa na Idara ya Watu Wenye Ulemavu kama ifuatavyo:-

i. Ofisi imehudhuria Mikutano ya kupitia na kuandaa mpango kazi na Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya Afrika Mashariki iliofanyika Dar es Salaam na Kampala, Uganda;
ii. Ofisi imetoa elimu na kuhamasisha jamii juu ya upatikanaji wa haki na fursa kwa Watu Wenye Ulemavu kupitia vipindi vya redio na televisheni, midahalo ya wanafunzi pamoja na mikutano iliyofanywa kwa taasisi za umma na binafsi, vikundi vya watu

wenye ulemavu pamoja na kuzitembelea familia zenye watu wenye ulemavu Unguja na Pemba na;

iii. Ofisi kwa kushirikiana na watu binafsi imewapatia visaidizi Watu Wenye Ulemavu 48 (21 wanawake na 27 wanaume) Unguja na Pemba. Visaidizi hivyo ni pamoja na Viti vya magurudumu mawili, viti vya chooni, magongo ya kutembelea na kusimamia.

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Programu ya Mipango na Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, kazi za Programu hizi zimetekelezwa na Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti na Uratibu wa Dawa za Kulevya kama ifuatavyo:-

i. Ofisi imerusha hewani vipindi vinne (4) vya redio kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya athari za Dawa za Kulevya, kufanya ziara za utoaji taaluma kwenye Skuli 38 ambapo jumla ya wanafunzi 1620 (Wanawake 913, Wanaume 707) walipatiwa taaluma hiyo. Pia ziara kama hizo zimefanyika kwenye Shehia 16 za Unguja na Pemba;

ii. Ofisi imezipatia ruzuku nyumba 13 za Makaazi ya Vijana walioacha matumizi ya Dawa za Kulevya (*Sober Houses*) na;

iii. Ofisi kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na wadau wengine imeandaa muongozo wa kuwazawadia watoa taarifa kuhusu uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya ambapo muongozo huo unasubiri vikao vya Tume kwa ajili ya kupatiwa mapendekezo.

TUME YA UKIMWI

Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa Ukimwi

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Ukimwi

Mhe. Spika, kazi za Programu hizi zimetekelezwa na Tume ya UKIMWI kama ifuatavyo:-

i. Ofisi kupitia Tume ya UKIMWI imetoa mafunzo ya Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar (Nam.18 ya mwaka 2013) kwa wadau mbali mbali. Aidha, Ofisi imetoa mafunzo kwa Viongozi 50 wa Taasisi za Kidini za Kiislamu na Kikiristo Unguja na Pemba juu ya muongozo wa Taasisi za Kidini wa masuala ya UKIMWI na afya ya uzazi kwa lengo la kuutambua muongozo huo na kuufanyia kazi;
ii. Ofisi imeandaa Mkakati wa Tatu wa Taifa wa UKIMWI kwa mwaka 2016/2020 kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali ambao walitoa maoni ya vipaumbele, shabaha na dira ya mkakati huo;
iii. Ofisi imeandaa Jarida la JIHADHARI kwa kuchapisha nakala 5000 na kusambazwa.
iv. Ofisi imefanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za UKIMWI ambapo ilifanya ziara kwa wadau 16 na Shehia 49 Unguja na Pemba zinazotekeleza shughuli mbali mbali za UKIMWI na;
v. Ofisi imetoa elimu kwa jamii juu ya masuala ya UKIMWI kupitia vipindi vya redio, filamu, maonyesho ya sanaa pamoja na kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha vijana wenye ulemavu wa uziwi 60 na mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 28 kutoka makundi maalum juu ya mbinu za kujiongezea kipato ili kuepukana na tabia hatarishi.

UTEKELEZAJI KIFEDHA

Mhe. Spika, Utekelezaji kifedha kwa Idara na Taasisi hizi mbili ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 289,782,000 kwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya Shilingi 25,680,000 zimetumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 8.8.
Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 544,383,451 kwa Tume ya UKIMWI. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya Shilingi 343,711,200 zimetumika ambazo ni sawa na asilimia 60.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 351,218,753 kwa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya Shilingi 237,449,000 zimetumika ambazo ni sawa na asilimia 70.

BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya Muundo wa Serikali yaliyofanyika, Programu zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Taasisi zake zimeongezeka kutoka programu kuu nane (8) na programu ndogo 14 hadi kufikia programu kuu kumi na mbili (12) na programu ndogo ishirini na nne (24). Zifuatazo ni Programu Kuu:

i. Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais;
ii. Uratibu wa shughuli za Serikali;
iii. Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa;
iv. Mipango na Utawala;
v. Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali;
vi. Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi;
vii. Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi;
viii. Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;
ix. Udhibiti wa Dawa za Kulevya;
x. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya;
xi. Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI na;
xii. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 35,992,076,000 kwa ajili ya kutekeleza program hizo kumi na mbili (12).

Programu ya kwanza: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais (C011)

Mhe. Spika, lengo la Program hii ni kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais. Matarajio ya muda mrefu ni kuimarika kwa Ofisi hii na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kuratibu kazi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ikiwemo ziara za ndani na nje ya nchi, mikutano na Mabalozi wa nchi mbali mbali, Wawakilishi wa Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na mikutano na wananchi ya kusikiliza kero na malalamiko yao.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Faragha kupitia Programu ya (C011) ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kuimarisha Ofisi ya Faragha kwa kuendelea kuratibu ziara mbali mbali za ndani na nje ya nchi;
b) Kuimarisha uhusiano mwema na nchi rafiki kwa kuongeza mashirikiano kwa kukaribisha wageni na Mabalozi wa nchi mbali mbali wa Kitaifa na Kimataifa;
c) Kuratibu na kutekeleza ahadi zinazolenga kuleta maendeleo katika jamii;
d) Kuyafanyia matengenezo makubwa Makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yaliyoko Dar es Salaam na Dodoma pamoja na kuimarisha huduma za usafiri na;
e) Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi watatu (3) wa Ofisi ya Faragha katika kiwango cha Diploma pamoja na kuwapatia stahiki za likizo wafanyakazi tisa (9).

Programu ya Pili: Uratibu wa shughuli za Serikali (C012)

Mhe. Spika, programu hii lengo lake kubwa ni kuweka mfumo imara na endelevu kwa Uratibu wa Shughuli za Serikali, ambapo matarajio ya muda mrefu ni kutoa huduma bora za Serikali kwa jamii.

Programu hii ina programu ndogo tano ambazo ni: -

i. Kukabiliana na Maafa;
ii. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa;
iii. Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano;
iv. Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar es Salaam na;
v. Usimamizi wa masuala ya watu wenye mahitaji maalum.

Programu ndogo C0121 Kukabiliana na Maafa

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla na baada ya kutokea. Huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu wa shughuli za Kukabiliana na Maafa ikiwemo kutoa mafunzo kwa jamii, kuwahudumia waathirika wa majanga na maafa pamoja na kuandaa na kutoa miongozo inayosimamia utekelezaji wa kazi za maafa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kupitia Programu ndogo (C0121) imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kufanya tathmini na kutoa mafunzo ya Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa kwa Shehia 50 za Unguja na Pemba;
b) Kuijengea uwezo Kamisheni katika kujikinga, kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa;
c) Kuandaa Kanuni ya Sheria ya Kukabiliana na Maafa Namba 1 ya mwaka 2015 na;
d) Kuendelea kuandaa na kutoa miongozo inayosimamia utekelezaji wa kazi za maafa.

Programu ndogo C0122: Uratibu wa Shughuli za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa ina lengo la kuwa na Sherehe zenye hadhi na kudumisha historia na kumbukumbu za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa shughuli za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kupitia Programu ndogo (C0122) ya Uratibu wa Shughuli za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kuandaa mazingira mazuri ya Ofisi na utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi na kuendelea kulipia gharama za masomo kwa wafanyakazi wawili (2);
b) Kuratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar;
c) Kuratibu Hitma na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume na Viongozi wengine waliotangulia mbele ya haki;
d) Kuratibu ushiriki wa Viongozi na wananchi wa Zanzibar katika maadhimisho na sherehe za Kitaifa zitakazofanyika nje ya Zanzibarna;
e) Kukamilisha mapitio ya Sheria Namba 10 ya mwaka 2002 ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa.

Programu ndogo (C0123): Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano (C0123) imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za Serikali;
b) Kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya 2015 hadi 2020;
c) Kuratibu shughuli za Muungano na Miradi ya Muungano ndani ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) na;
d) Kuratibu shughuli za utafiti nchini.

Programu Ndogo C0124: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dar es Salaam

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar es Salaam ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa Taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara. Huduma inayotolewa ni Uratibu wa shughuli za Serikali (SMZ) Dar es Salaam.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali Dar es Salaam kupitia Programu ndogo (C0122) imepanga kufanya yafuatayo:-

a) Kuimarisha mashirikiano baina ya Ofisi ya uratibu shughuli za Serikali Dar es Salaam na Taasisi za SMZ na SMT, Ofisi za Kibalozi na Taasisi za Kimataifa;
b) Kukamilisha muundo mpya wa kitaasisi na kiutumishi wa Ofisi;
c) Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Ofisi kwa ununuzi wa vifaa vya Ofisi na samani;
d) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wawili (2) ili kuwaongezea utaalamu na;
e) Kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Dar es Salaam.

Programu Ndogo C0125: Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu:

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu ambapo lengo lake ni kupatikana kwa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kuimarishwa ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu, uwezeshwaji wa watu wenye ulemavu na kukuza uelewa wa jamii juu ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Watu Wenye Ulemavu kupitia Programu ndogo (C0125) ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu imepanga kutekeleza yafuatayo:

a) Kupitia upya Sheria Nam. 9 2006 (HAKI NA FURSA) ya Watu wenye Ulemavu;
b) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Watu wenye Ulemavu;
c) Kusimamia upatikaji wa Haki na Fursa sawa za Watu wenye Ulemavu;
d) Kufanya ukondoeshwaji, kuwajengea uwezo Watu wenye Ulemavu na taasisi zao na kufanya uhamasishaji wa jamii juu ya masuala ya Watu wenye Ulemavu na;
e) Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Programu ya Tatu: Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa (C013)

Mhe. Spika, Programu hii lengo lake ni kukiimarisha Kiwanda cha Upigaji Chapa ili kutoa huduma bora za machapisho na kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:

a) Kutoa huduma bora za uchapishaji wa nyaraka na Sheria za Serikali;
b) Kutangaza na kushajiisha uelewa wa utoaji huduma za Uwakala na Kiwanda kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja na mapato;
c) Kufanya maandalizi ya uanzishaji wa Bohari Kuu ya vifaa vya Ofisi na;
d) Kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa lengo la kutoa machapisho bora yanayoendana na teknolojia ya kisasa ya uchapishaji.

Programu ya Nne: Mipango na Utawala (C014)

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za Ofisi. Matokeo yanayotarajiwa ni kuimarika mipango na utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wafanyakazi na wadau mbali mbali wa Ofisi hii. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni:-

i. Uongozi na Utawala;

ii. Mipango, Sera na Utafiti na;
iii. Ofisi Kuu Pemba.

Programu ndogo (C0141): Uongozi na Utawala

Mhe. Spika, Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni matumizi bora ya rasilimali, wafanyakazi wenye ujuzi na uzoefu na ufanisi katika utendaji kazi. Huduma zinazotolewa ni kusimamia maslahi ya wafanyakazi na matumizi bora ya rasilimali za Ofisi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi kupitia programu ndogo ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

a) Kusimamia shughuli za uendeshaji wa Ofisi za kila siku ikiwemo malipo ya umeme, maji, mawasiliano, mafuta, vifaa vya usafi pamoja na vifaa vya kufanyia kazi;
b) Kufanya ukarabati mdogo katika jengo kongwe la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Vuga;
c) Kuimarisha huduma za usafiri;
d) Kuimarisha Kitengo cha kumbukumbu kwa kukifanyia ukarabati pamoja na kuwekwa samani za kisasa na vifaa vya kufanyia kazi;
e) Idara inaendelea kufanya mapitio ya mahitaji ya mafunzo (*Training Need Assessment -TNA*);
f) Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi;
g) Kufanya semina moja juu ya Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 na Semina moja ya kujikinga na maambukizi na madhara ya UKIMWI pamoja na maradhi yasioambukiza kwa wafanyakazi 100na;
h) Kuandaa vikao vinne (4) vya Kamati ya Uongozi, Vikao vinne (4) vya Kamati ya Ukaguzi, Vikao vinne vya Bodi ya Zabuni pamoja na kuendelea kufanyia mapitio daftari la mali za Serikali kwa mujibu wa Sheria za Udhibiti wa mali za Serikali

Programu ndogo (C0142): Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, Programu hii ndogo ina lengo la kuandaa na kusimamia Mipango na Bajeti na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Ofisi ya

Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwa na mipango endelevu na yenye kuleta maendeleo. Huduma inayotolewa ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mipango na Bajeti.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi kupitia Programu ndogo (C0142) imepanga kufanya yafuatayo:-

a. Kuandaa Bajeti na kutayarisha Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufanya ziara nne (4) za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu/ Miradi ya Maendeleo inayotekeleza chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
b. Kusimamia tafiti zinazotekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
c. Kuratibu Sera na Sheria zinazotayarishwa kwa ajili ya shughuli zinazotekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
d. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi yanayohusu ufuatiliaji na tathmini kwa kazi za kawaida na maendeleo na wafanyakazi watatu (3) mafunzo ya muda mrefu;
e. Kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria kupitia Mfuko wa Dunia *(Global Fund).*

Programu ndogo (C0143): Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, lengo kuu la Program hii ndogo ni Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba. Matokeo yanayotarajiwa ni utendaji na utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba kwa ufanisi. Huduma inayotolewa ni Uratibu wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi Kuu Pemba itatekeleza Lengo la Kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba kama ifuatavyo:-

a) Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
b) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4);
c) Kuandaa mipango ya Ofisi na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2017/2018;
d) Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
e) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Pembana;

f) Kutangaza huduma za Kiwanda kwa ajili ya kuongeza idadi ya wateja na mapato.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pia inaratibu shughuli za Baraza la Wawakilishi, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya *UKIMWI*, ambazo nazo zina Programu Kuu na Programu Ndogo kama ifuatavyo:-

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi linatekeleza Program kuu mbili (2) ambazo ni:-

Programu ya tano: Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali

Mhe. Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatekelezwa Zanzibar, ambapo matarajio yake ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Huduma zinazotolewa ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia utendaji wa Taasisi za Serikali na kupitisha bajeti ya Serikali.

Programu ya sita: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika, Programu hii ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanya kazi wa Ofisi ya Baraza, ambapo matarajio yake ya muda mrefu ni kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Ofisi. Huduma zinazotolewa ni kuwapatia Wajumbe na wafanyakazi wa Baraza huduma na stahiki zao, kuimarisha uwezo wa Wajumbe na watendaji na kuimarisha mazingira ya kazi ya Ofisi ya Baraza.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 Baraza la Wawakilishi limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kufanya mikutano minne ya Baraza;
b) Kuziwezesha Kamati zake za kudumu kufanya kazi;
c) Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wake;
d) Kuendeleza mahusiano na vyombo vyengine vya Mabunge, Kanda ya Afrika na ngazi ya Kimataifa;
e) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wajumbe ili waweze kutekeleza majukumu yao;

f) Kuendelea kutoa elimu kwa Umma inayohusu majukumu ya Baraza kupitia Redio na Televisheni na;
g) Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya majengo na kumbi za mikutano.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi inasimamia Programu kuu mbili kama zifuatazo:-

Programu ya saba: Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi

Mhe. Spika, Programu hii ina jukumu la kukuza Demokrasia na Umoja wa Kitaifa ambayo matarajio yake ya muda mrefu ni kuwa na Uchaguzi Huru na wa haki na wenye kufuata misingi ya kisheria. Huduma zinazotolewa ni kufanya Uchaguzi Mkuu, Chaguzi ndogo na Kura ya maoni, Kufanya Uchambuzi wa Idadi, Majina na Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi, Kuratibu na kutoa elimu ya Wapiga Kura pamoja na Uandikishaji wa Wapiga Kura na Uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia programu hii imepanga kuendesha Chaguzi Ndogo.

Programu ya nane: Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

Mhe. Spika, Programu hii ya pili ina jukumu la kuimarisha usimamizi wa mwenendo wa Shughuli za Uchaguzi, ambayo matarajio yake ya muda mrefu ni uendeshaji bora wa kazi za Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Programu hii inasimamia programu ndogo mbili nazo ni:-

i. Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na;
ii. Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina lengo la kuimarisha Usimamizi wa mwenendo wa Shughuli za Uchaguzi. Matokeo yanayotarajiwa ni uendeshaji bora wa kazi za Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Huduma zinazotolewa na program hii ndogo ni kuimarisha mazingira bora ya kufanyia

kazi, kuimarisha maslahi ya wafanya kazi na kuwajengea uwezo wafanya kazi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba ina lengo la kuimarisha Usimamizi wa mwenendo wa Shughuli za Uchaguzi Pemba. Matokeo yanayotarajiwa ni uendeshaji bora wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Huduma zinazotolewa na program hii ndogo ni kuimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi ya Tume ya Uchaguzi Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 Tume ya Uchaguzi kupitia programu hii imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kuweka na kusimamia mazingira mazuri ya utendaji kazi na;
b) Kuwapatia mafunzo wafanya kazi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA:

Mhe. Spika, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ina jukumu kuu la kuratibu mapambano dhidi ya matumizi, biashara na usafirishaji wa dawa za kulevya, kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya pamoja na tiba na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa hizo. Taasisi hii imepangiwa kusimamia Program Kuu mbili kama ifuatavyo:-

Program ya tisa: Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni:-

a) Kuzijengea uwezo nyumba za upataji nafuu *(sober houses);*
b) Kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya katika bandari zilizo na zisizo rasmi;
c) Kuratibu na kuendeleza mapambano juu ya uingizaji, usambazaji na usafirishaji wa dawa za kulevya na;
d) Kupunguza matatizo ya athari za utegemezi wa dawa za kulevya.

Programu ya kumi: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuweka mazingira mazuri ya kazi za ofisi. Huduma zinazotarajiwa ni upatikanaji wa huduma na vitendea kazi,

kujenga uwezo wa wafanya kazi na usimamizi wa matumizi ya fedha pamoja na kukuza uwajibikaji.

Mhe. Spika, Kazi za programu hii zinatekelezwa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na ina program ndogo mbili ambazo ni:

i. Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na;
ii. Uratibu wa Masuala ya Dawa za Kulevya Pemba.

Mhe. Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni:-

a) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na kusimamia utekelezaji wake;
b) Kujenga uwezo wa wafanyakazi katika mapambano ya dawa za kulevya na;
c) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanya kazi.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika, Tume ya Ukimwi ina jukumu la kuratibu masuala ya *UKIMWI* hapa Zanzibar, ambapo imepangiwa kusimamia Programu Kuu mbili kama ifuatavyo:-

Programu ya kumi na moja: Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI

Mhe. Spika, Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni:

i) Uratibu wa muitiko wa Taifa wa UKIMWI na;
ii) Mawasiliano na Utetezi wa Masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na programu hii ni:

a) Kuongeza uelewa wa masuala ya *UKIMWI* na afya ya uzazi na matumizi ya huduma kwa makundi ya vijana na rika baleghe (10 – 24);
b) Kujenga uwezo wa wadau na jamii kutekeleza Mkakati wa Tatu utakaochangia kudhibiti kuenea UKIMWI, udhalilishaji wa kijinsia na kuimarisha masuala ya afya ya uzazi;
c) Kutekeleza programu za ushawishi na mawasiliano kwa ubunifu zaidi na kukabiliana na changamoto mpya;

d) Kusimamia mfumo wa ufuatiliaji na tathmini uendelee kufanya kazi;
e) Kujenga uelewa wa jamii wa Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya *UKIMWI* Nam. 18 ya mwaka 2013 na;
f) Kuendeleza maandalizi ya uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa *UKIMWI*.

Program ya kumi na mbili: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuweka mazingira mazuri ya kazi za ofisi. Huduma zinazotarajiwa ni upatikanaji wa huduma na vitendea kazi, kujenga uwezo wa wafanyakazi na usimamizi wa matumizi ya fedha, uwazi na uwajibikaji. Programu hii imepangiwa kusimamia programu ndogo mbili ambazo ni: -

i. Uratibu wa masuala ya *UKIMWI* Pemba na;
ii. Utawala na uendeshaji Unguja.

Mhe. Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni:-

a) Kununua vifaa, huduma na kufanya matengenezo ya majengo, vifaa na gari;
b) Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ufanisi wa kazi;
c) Kufanya mapitio ya Muongozo wa Fedha na Uhasibu wa Tume na kutoa mafunzo ya mfumo wa kiuhasibu kwa wahusika na ;
d) Kutekeleza programu ya afya kwa wafanya kazi na familia zao.

Mhe. Spika, kwa muhtasari wa Programu na Programu ndogo za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake **Angalia Kiambatisho Nam 3.**

MGAO WA FEDHA KWA PROGRAMU

Mhe. Spika, mgao wa fedha kwa Programu kumi na mbili (12) za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ni kama ifuatavyo: -

Programu ya kwanza: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **756,466,000** kwa kazi za kawaida.

Programu ya pili: Uratibu wa shughuli za Serikali. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **3,028,975,000** kwa kazi za kawaida na Shilingi **8,330,450,000** kwa kazi za maendeleo (Shilingi 210,000,000 za SMZ na Shilingi 8,120,450,000 ni mchango wa Wahisani).

Programu ya tatu: Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **873,940, 000** kwa matumizi ya kawaida.

Programu ya nne: Mipango na Utawala. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **1,857,468,000** kwa kazi za kawaida na Shilingi **1,000,000,000** kwa kazi za maendeleo.

Programu ya tano: Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **6,542,950,000** kwa kazi za kawaida.

Programu ya sita: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **10,595,550,000** kwa kazi za kawaida.

Programu ya saba: Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **1,174,812,000** kwa kazi za kawaida.
Programu ya nane: Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **185,388,000** kwa kazi za kawaida.

Programu ya tisa: Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **88,813,000** kwa kazi za kawaida.

Programu ya kumi: Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **351,087,000** kwa kazi za kawaida.

Programu ya kumi na moja: Kuratibu Muitiko wa Taifa wa *UKIMWI*. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **222,589,000** kwa kazi za kawaida na Shilingi **519,076,000** kwa kazi na maendeleo (Shilingi 20,000,000 fedha za SMZ na 499,076,000 mchango wa Wahisani).

Programu ya kumi na mbili: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya *UKIMWI*. Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **464,511,000** kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, jumla ya makisio kwa Programu zote 12 za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi **35,992,076,000. Kiambatisho Nam. 3.**

UKUSANYAJI WA MAPATO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepanga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 806,126,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

Wakala wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali: TShs.793,766,000
Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa: TShs. 12,360,000

HITIMISHO

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo, sasa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru pia watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Joseph Abdallah Meza na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ahmad Kassim Haji kwa juhudi zao katika kutekeleza majukumu yaliyo mbele yetu.

Mhe. Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na shukurani maalumu kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano, ushauri na maelekezo waliyotupa katika kukamilisha bajeti. Aidha, napenda kuwashukuru sana Washirika wa Maendeleo, *(Development Patners)* na nchi marafiki ambazo zinaendelea kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Ofisi yangu na ya nchi kwa jumla katika mwaka wa fedha 2015/2016. Miongoni mwao ni: Benki ya Dunia, Clinton Foundation, China, FAO, Finland, Norway, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI *(Global Fund),* Oman, UNAIDS, USAID, UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP na WIPO.

Vile vile naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri MKuu kwa ushirikiano wao mkubwa na Ofisi yangu. Pia nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali, Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia Serikali katika kutoa huduma za jamii na kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Pia nawashukuru sana wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza hotuba yangu hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **35,992,076,000** kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza programu nilizozielezea hapo juu. Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

i.	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	TShs: 15,847,300,000/-
ii.	Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	TShs: 17,138,500,000/-
iii.	Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	TShs: 1,360,200,000/-
iv.	Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya	TShs: 439,900,000/-
v.	Tume ya UKIMWI Zanzibar	TShs: 1,206,176,000/-
	Jumla:	**TShs.35,992,076,000/=**

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji wake mzuri kabisa ambao ameutoa hivi punde. Sasa napenda nichukue nafasi sasa kumwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Omar Seif Abeid ili nae sasa aje awasilishe.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, nachukua fursa hii adhimu ulionipa ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa neema zake za uzima na afya njema aliotupa sisi waja wake na kwa kufanya hivyo kuwa tunatekeleza jukumu letu moja kuu tunalotakiwa la kuzishukuru neema zake Mwenyezi Mungu Mtukufu.Nasi hatuna budi nianze kutoa maoni ya kamati kwa shukurani hizo kwa Mwenyezi Mungu wetu mtukufu.

Mhe. Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwako wewe kwa kupata ridhaa ya wajumbe na hatimae kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili. Lakini pia niwapongeze Wajumbe wote wa Baraza hili kwa ushindi wa kishindo

walioupata kupitia majimboni mwao, viti maalum na wale wateule wa Mhe. Rais, lakini nisisahau kuwapongeza kwa dhati Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo. Imani ya Mhe. Rais kwao ni kubwa sana na yenye matumaini ya kuisaidia nchi yetu kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Mhe. Spika, sitaacha kuusiana sote kuwa "Cheo ni Dhamana". Ni vyema tukakumbuka pia kuwa tumebeba dhima kubwa kwa Mwenyezi Mungu wetu na kwa wananchi tunaowaongoza, na kwamba kama tutakwenda kinyume na dhamana hiyo, tutakuwa tumetenda kosa na kubeba mzigo mzito sana shingoni mwetu.

Mhe. Spika, kamati yangu imepewa jukumu la kupitia bajeti ya wizara mbili, ambazo zote ni Ofisi za Viongozi Wakuu wa Taifa hili; Ofisi ya kwanza ni ya mwenyewe Mhe. Rais ambayo ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, muundo wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais unajumuisha mafungu matano makuu:

1. Fungu la C01 la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
2. Fungu la C02 ni la Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;
3. Fungu la C03 ni la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;
4. Fungu la C04 ni la Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya;na
5. Fungu la mwisho la C05 ni la Tume ya Ukimwi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati yetu imeyafanyia kazi mafungu yote hayo kwa siku moja, pamoja na kuwa, vitabu vya bajeti tumevipokea siku ya Jumapili ya tarehe 08/05/2016 saa 6 mchana, na sisi tuliijadili bajeti hii siku ya Jumatatu ya tarehe 09/05/2016 saa 3:00 asubuhi. Aidha, kamati zako nyingi ikiwa ni pamoja na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, imepokea kitabu cha bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali siku hiyo hiyo.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba bajeti ndio msingi wa serikali. Kwa hivyo, kukusanya mapato na kutumia fedha hizo kwa shughuli za kawaida na zile za maendeleo kwa ajili ya wananchi wake. Kwa hivyo, sisi kama wawakilishi wa wananch, na kwa sababu sisi ndio wasemaji wakuu wa wananchi wetu, ni vyema na busara kwa serikali yetu kuangalia zile kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi haraka iwezekanavyo ili kuondoa baadhi ya malalamiko ya kero hizo.

Mhe. Spika, kamati zako ikiwa ni pamoja na kamati yetu, ndio eneo pekee la wajumbe wako kupata fursa ya kuchambua kwa undani Bajeti ya Serikali na Wizara zake, ili wajumbe wapate wasaa wa uchambuzi wa kina. Kwa hiyo, ni vyema kwa Wajumbe wa Kamati wapatiwe vitabu vya bajeti kwa wakati na wapewe muda wa kutosha wa kuijadili na kuipitisha bajeti za wizara inazozisimamia, na sio kufanya mambo kwa kuripua, au kama vijana wa leo wanavyoita "Zima Moto".

OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS (FUNGU C01)

Mhe. Spika, niendelee kueleza kuwa, kamati yetu imeichambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo inaundwa na idara zifuatazo:-

- Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais;
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
- Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya
- Muungano;
- Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar-es-Salaam;
- Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa;
- Idara ya Watu Wenye Ulemavu, na
- Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, katika idara nilizozitaja Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inakusudia kuifanya Idara ya Maafa kuwa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, suala kubwa ambalo sisi Wajumbe wa Kamati tunalojiuliza ni vipi ofisi hii itaweza kujiendesha na kuleta ufanisi wakati hali halisi ya bajeti yake ya mwaka uliopita haikupatikana kwa kiwango cha ukamilifu, ambapo mahitaji ya mwaka huu ni makubwa zaidi kuliko mahitaji ya mwaka uliopita.

Mhe. Spika, ofisi hii mwaka jana, bila ya kuzingatia taasisi zinazojitegemea zilizochini yake, ilitengewa Tsh. 5,066,700,000 kwa kazi za kawaida na Tsh. 100,000,000 kwa kazi za maendeleo, lakini hali halisi hadi kufikia *March* mwaka huu, fedha za maendeleo zilizopatikana ni asilimia 50 tu, wakati fedha za maendeleo kwa mwaka huu zimeongezeka na kuwa Tsh. 8,330,450,000 wakati utendaji wa vianzio vyake vya mapato unasuasua.

MAPATO YATAKAYOKUSANYWA NA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepewa jukumu la kukusanya Tsh. 793,766,000 kwa mwaka huu wa fedha, ikiwa nyongeza ya Tsh. 181,406,000 ya makusanyo ya mwaka jana ambayo ilikisiwa kukusanywa Tsh. 612,360,000. Hata hivyo, uhalisia wa makusanyo hayo ya mwaka jana ilikuwa Tsh. 289,325,120 kukiwa na upungufu wa Tsh. 323,034,880/- ya makusanyo yaliyotarajiwa.

Mhe. Spika, idara zilizopewa jukumu la makusanyo hayo mwaka jana na mwaka huu ni hizo hizo mbili; Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Aidha, mwaka jana Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ilitarajiwa kukusanya Tsh. 3,000,000 kutokana na ukodishaji wa vifaa na Tsh. 9,360,000 kwa ajili ya mapato ya ukodishwaji wa milango iliopo Mwanakwerekwe.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha, Idara hii ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa haijaongeza chanzo chochote cha mapato bado inategemewa kukusanya Tsh. 9,360,000 kama ilivyokisiwa mwaka jana kwa kukodisha majengo ya serikali, kwa maana kukodisha milango ya maduka iliyopo Mwanakwerekwe. Aidha, idara hii bado inategemewa kukusanya fedha zile zile zilizokisiwa mwaka jana Tsh. 3,000,000 kwa ukodishaji wa vifaa ambavyo ni viti na mashamiana. Aidha, kamati inaomba kupitia wizara husika itoe ufafanuzi vipi wanaweza kufikia lengo la mapato yake ikiwa kama hamna vianzio tofauti vya mapato.

Mhe. Spika, kamati inaitaka Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kuongeza makusanyo ya mapato, kwani hivi sasa serikali yetu lazima itegemee kodi ya ndani kuliko kutegemea wahisani wa maendeleo. Aidha, kamati yetu imesikitishwa na hoja zilizotolewa na wizara kuwa wameshindwa kuongeza kodi za maduka yao yaliyopo Mwanakwerekwe kwa sababu tu baadhi ya waheshimiwa ikiwa ni pamoja na waliokuwa Wajumbe wa Kamati hii ya Baraza lililopita na wakubwa wengine serikalini wamefuatwa na wafanyabiashara waliokodishwa maduka hayo wakililia hali na kutaka kupunguziwa kodi.

Mhe. Spika, Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali mwaka uliopita ilikisiwa kukusanya Tsh. 600,000,000 kwa ada ya mauzo ya uchapishaji. Na mwaka huu mapato hayo yameongezwa kwa Tsh.181,406,000 na kufikia Tsh.781,406,000. Kamati yetu inazipongeza juhudi hizo za kuongeza

makusanyo hayo. Lakini pamoja na pongezi zetu, tunapenda ieleweke kuwa, wateja wakuu wa idara hii ni Taasisi za Serikali ambazo kwa ufupi nyingi zao hazilipi madeni yao kwa wakati au hazilipi kabisa.

Mhe. Spika, kamati yetu inafahamu kuwa Ofisi ya Makamu wa Pili inakusudia kuifanya Idara hii ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, lakini bado inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na uwezo wa kujiendesha kutokana na uchache wa mapato inayoyapata.

Mhe. Spika, tunaitaka serikali ihakikishe kuwa idara na taasisi zake zote zinazodaiwa na Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali zinalipa madeni yao kwa wakati. Aidha, kamati inaitaka idara hii ihakikishe inafuata mwelekeo wa Shirika la Umeme, kuwa taasisi zote zisizolipa madeni yao wasizipe huduma kabla ya kulipa madeni yao, na ihakikishe inafuatilia kwa kuwaandikia barua wakuu wote wa taasisi zinazozidaiwa kuanzia tarehe ya uwasilishaji wa hotuba yetu leo hii.

Mhe. Spika. pamoja na juhudi zilizochukuliwa na serikali yetu za kuiboresha idara hii kuipatia mitambo ya kisasa ya uchapaji, kamati yetu inaishauri wizara kuwapatia mafunzo ya kutosha watendaji wakuu wa Idara hii ya Upigaji Chapa na kuwaalika Watendaji Wakuu wa Shirika la Nyumba la Tanzania ili waweze kubadilishana mawazo kwa lengo la kuimarisha idara yetu hii iweze kubadilika na kutekeleza vyema kazi zake.

Mhe. Spika, kamati yetu inaishauri Idara ya Upigaji Chapa na Mpigaji Chapa Mkuu wa Serikali izingatie na iongeze ustadi wa kufanya kazi za '*graphic'* na '*design'*, kwani hivi sasa nchini mwetu kuna Makampuni na Taasisi mbali mbali zinafanya kazi hiyo kwa ufanisi, hali ambayo kama idara yetu hii haitojipanga vyema kuingia katika soko la ushindani itakosa wateja na hivyo itashusha makusanyo yake ya mapato.

MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaomba Tsh. 6,517,000,000 kwa kazi za kawaida ambazo zinatarajiwa kutumika kwa kuzingatia propramu kuu tano na programu ndogo kumi kama zifuatazo:

Namba ri	Programu Kuu	Programu Ndogo
C01011	Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais
C0102	Uratibu wa Shughuli za Serikali	Kukabiliana na Maafa
		Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa
		Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano
		Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar-es- Salaam
		Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu
C0103	Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa	Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa
C0104	Uongozi na Utawala	Uongozi na Utawala
		Mipango, Sera na Utafiti
		Ofisi Kuu Pemba

PROGRAMU KUU YA URATIBU WA SHUGHULI ZA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, programu kuu hii na programu yake ndogo inaombewa Tsh. 756,566,000 kwa matumizi yake ya kawaida, ambapo fedha hizo zitatumika kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao za mishahara, posho mbali mbali na michango ya *ZSSF*; kuimarisha huduma za usafiri, kununua vifaa vya kuandikia na vifaa vyengine muhimu vya ofisi; kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; kulipa huduma za ofisi; kufanya ukarabati wa majengo na kugharamia uendeshaji na huduma za ofisi.

Mhe. Spika, wakati kamati yetu ilipokuwa inapitia programu kuu hii, ilihitaji ufafanuzi wa matumizi ya Tsh. 120,000,000 ya ununuzi wa gari na kuelezwa kuwa, fedha hizo zitatumika kwa ununuzi wa gari ya kutoa huduma za jikoni kwa ajili ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Aidha, fedha hizo ni makisio tu na sio halisi, hali ambayo itaifanya ofisi kuweza kununua gari inayoihitaji yenye sifa na hadhi ya huduma inazotarajiwa kuzitoa.

Mhe. Spika, kamati yetu inaendelea kuikumbusha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba ni jukumu lake la kufanya manunuzi kwa kuzingatia sheria za nchi na hali ya kipato katika ununuzi wa gari hiyo. Aidha, iwapo itatokezea fedha zilizotengwa kuwa kidogo kwa mujibu wa gari inayohitajika, kamati yetu inaitaka Ofisi ya Makamu wa Pili kufuata taratibu za sheria ya fedha katika kufanya uhaulishaji kama inavyotakiwa na sio kufanya vyenginevyo.

PROGRAMU KUU YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, program kuu hii inaombewa Tsh.11,359,476,000 ambapo proramu ndogo ya kwanza ya kukabiliana na maafa itatumia Tsh. 850,917,000 kwa kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa, programu ndogo ya pili ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa itatumia jumla ya Tsh. 1,037,082,000 kwa ajili ya uratibu wa shughuli za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, pamoja na kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Programu ndogo ya tatu katika programu kuu hii ni shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano itakayotumia jumla ya Tsh. 8,561,838,000 na programu ndogo ya shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar-es-Salaam ambayo itatumia jumla ya Tsh. 447,517,000 na ya mwisho katika programu kuu hii ni usimamizi wa masuala ya watu wenye Ulemavu itakayotumia jumla ya Tsh. 462,121,000.

Mhe. Spika, kamati yetu imeelezwa kuwa, wizara na serikali kwa ujumla inakusudia kuifanya Idara ya Kukabiliana na Maafa inayoisimamia Programu Ndogo ya Programu Kuu hii, kuwa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa badala ya kubakia Idara ya Kukabiliana na Maafa kama ilivyo sasa.

Mhe. Spika, pamoja na adhima nzuri ya serikali, kamati yetu imeingiwa na khofu juu ya uwezo wa idara hii wa kukabiliana ipasavyo na maafa wakati itakapokuwa Kamisheni, ikizingatiwa kwamba idara hiyo haina vifaa vya kutosha ambavyo ni vya kwake wenyewe hasa vifaa vya uokozi vya kukabiliana na maafa pindi yanapotokea.

Mhe.Spika, kamati yetu imeelezwa kuwa, idara ina vifaa vya kibinaadamu vya kukabiliana na maafa yanapotokea ambapo sasa ina maghala mawili ya kuhifadhia vifaa hivyo, moja likiwa Pemba na jengine Unguja. Wakati vifaa vyote vya Uokozi viko chini ya Taasisi nyengine za Serikali, Idara hii ina orodha tu ya vifaa na huviomba pale inapotokea dharura ya kufanya hivyo. Jambo hili ni vyema likaangaliwa upya kwa idara inayohusika kuwa na vifaa vyake kamili, kwa mfano Boti za Kuokolea, Maboya na vifaa vyengine muhimu vya kukabiliana na maafa pindi yanapotokea.

Kamati yetu imepata hofu ya utekelezaji wa kazi za idara hii kwani hali hairidhishi hata kidogo, kwa kuzingatia misaada ambayo idara hii iliipata wakati Meli ya *Mv. Spice Islander* iliyokuwa inatokea Unguja kwenda Pemba ilipozama na meli nyengine iliyokuwa ikitokea Dar-es-Salaam kuja Unguja. Hali hii ni ya kusikitisha sana kwani tunaamini kwamba, idara ingekuwa na vifaa vya kutosha maisha ya watu wengi zaidi yangeweza kuokolewa. Kwa hivyo, inapaswa sasa idara ikawa na vifaa vyake wenyewe vya uokozi, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa idara hiyo.

Mhe. Spika, kamati yetu imepata ufafanuzi wa Tsh. 3,890,000 za kutengeneza Kanuni za Sheria za Watu Wenye Ulemavu na kuelezwa kuwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu inaendelea na mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria yake ya Watu Wenye Ulemavu, (Nam. 9 ya mwaka 2006) kwa mashirikiano na Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati imearifiwa kuwa, baada ya kukamilika kwa marekebisho ya sheria hiyo na kupitishwa na Baraza hili, ndipo watakapoharakisha kukamilisha marekebisho ya kanuni ambayo wanatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, kamati yetu imefurahishwa na maelezo hayo na inaitaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na serikali kwa ujumla kutoa ushirikiano kikamilifu kwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu, ili waweze kufikia lengo hilo na kuleta ufanisi katika kusimamia haki za watu wenye ulemavu Zanzibar.

Progamu Kuu hii ina miradi mikuu miwili; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa utakaotumia jumla ya Tsh.270,000,000, ambapo Serikali itatoa Tsh.150,000,000 huku Wahisani wa Maendeleo (Shirika la Kimataifa la Maendeleo (*UNDP*) itatoa jumla ya Tsh.120,450,000. Aidha, mradi wa pili wa kusimamiwa chini ya Programu Kuu hii ni Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) utakaotumia Tsh. 8,060,000,000.

Mhe. Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inatarajiwa kutoa Tsh. 60,000,000 za Mradi wa *TASAF* huku Benki ya Dunia inatarajiwa kutoa jumla ya Tsh. 8,000,000,000. Fedha hizo zitatumika kwa kusimamia malipo kwa kaya masikini katika Shehia 240 Unguja na Pemba; kuratibu shughuli za *TASAF III* baina ya Zanzibar na Dar-es-Salaam, kuandaa mikutano miwili ya Kamati ya Uongozi; kuandaa mikutano miwili ya Kamati Tendaji; kuendesha shughuli za ofisi na kufanya malipo kwa Kaya Masikini 33,632 kwa Shehia za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kamati yetu inaendelea kuitaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kusimamia ipasavyo miradi hii ya *TASAF*, kwani wananchi wanapaswa kushirikishwa ipasavyo na miradi hii inatakiwa kuwa endelevu ili iweze kuleta tija kwa wananchi wetu kwa muda mrefu.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UPIGAJI CHAPA

Mhe. Spika, programu kuu hii ina programu ndogo moja ambayo ni hiyo hiyo ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa, ambayo imekisiwa kutumia jumla Tsh. 873,940,000 kwa shughuli ya kutoa huduma za upigaji chapa. Pamoja na juhudi na nia ya serikali kuifanya Idara hii ya Upigaji Chapa kuwa Wakala wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Kamati yetu inashangazwa na juhudi hizi bila ya kuweka mradi wowote wa kuinua utendakazi wa idara hii.

Pia, kamati yetu imesikitishwa na bajeti ndogo ya idara hii huku kwa mfano ikiuliza uwezekano wa Tsh. 2,500,000 kutumiwa kwa ajili ya ununuzi wa Honda, Vespa na *Ciao*, wakati vespa moja ndio hununuliwa kwa Tsh. 2,500,000. Je, huu ni ukweli kwamba fedha hizo zitakidhi kununua vyombo hivyo vyote vitatu.

PROGRAMU KUU YA UONGOZI NA UTAWALA

Mhe. Spika, Programu Kuu hii ina programu ndogo tatu na imekisiwa kutumia Tsh. 2,857,468,000. Programu ndogo ya Uongozi na Utawala itatumia Tsh. 2,042,593,000; Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti itatumia Tsh. 286,925,000 na Programu Ndogo ya Ofisi Kuu Pemba itatumia Tsh. 527,950,000.

Mhe. Spika, Propgramu Kuu hii ya Uongozi na Utawala itasimamia Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Kituo cha Kurekebisha Tabia kwa Watumiaji wa Madawa ya Kulevya, ambao utatumia Tsh.1,000,000,000, fedha ambazo zote kwa pamoja zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kununulia samani za ofisi kwa Tsh. 475,000,000; kugharamia ufuaji wa nguo Tsh. 275,000,000 na kutengeneza jiko Tsh. 250,000,000.

Mhe. Spika, kamati yetu inapendekeza kuwa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya ufuaji wa nguo Tsh. 275,000,000 zipunguzwe kwa asilimia 30 na badala yake fedha hizo zitakazopunguzwa zipelekwe katika Idara ya Mpigaji Chapa Mkuu wa Serikali. Kwa sababu fedha hizo ni nyingi sana kwa mujibu wa kazi zinazoainishwa za ufuaji wa nguo tu.

Mhe. Spika, kamati yetu itajitahidi sana kufuatilia utekelezwaji na usimamizi wa miradi yote iliyo chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, na kwa nafasi hii, Kamati inaitaka Ofisi hii kutekeleza ipasavyo miradi hiyo kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

BARAZA LA WAWAKILISHI (FUNGU C02)

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi linatekeleza Programu Kuu mbili. Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali ambayo ina programu ndogo moja iliyo sawa na Programu Kuu na Programu Kuu ya pili ni ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi yenye porgramu ndogo mbili. Programu ndogo ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi na Programu ndogo ya Afisi Kuu Pemba.

PROGRAMU KUU YA KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi linahitaji jumla ya Tsh. 17,138,500,000 kwa matumizi ya kawaida, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 375,900,000 kwa mwaka uliopita, ambapo fedha zilizoombwa zilikuwa Tsh. 16,762,600,000 kwa matumizi hayo ya kawaida, bila ya kuwa na mradi wowote wa maendeleo kama ilivyokuwa mwaka uliopita.

Mhe. Spika, kwa ajili ya kutekeleza programu kuu niliyoitaja hapo awali, Baraza la Wawakilishi linahitaji jumla ya Tsh. 6,542,950,000 zitakazotumika kwa kutunga sheria, kupitisha bajeti ya serikali na kusimamia taasisi za serikali.

PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA

Mhe. Spika, programu kuu hii inatarajiwa kutumia jumla ya Tsh. 10,595,550,000, ambapo jumla ya Tsh. 7,873,457,000 zitatumika kwa kutekeleza Programu ndogo ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi na jumla ya Tsh. 2,722,093,000 zitatumika kwa programu ndogo ya pili ya Afisi kuu Pemba.

Kamati yetu imepitisha bajeti ya Baraza la Wawakilishi kama ilivyoombwa, huku tukimuomba Katibu wa Baraza la Wawakilishi ambae ndie msimamizi Mkuu wa fedha hizi, kuzisimamia ipasavyo kwani tutakuwa wakali pale ambapo tutakapofuatilia matumizi na kugundua kuwa fedha hizo hazikutumika ipasavyo.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (FUNGU NAMBA C03)

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaombewa jumla ya Tsh. 1,360,200,000 kwa matumizi yake ya kawaida kwa mwaka huu wa fedha, kukiwa na upungufu wa Tsh. 43,800,000 wa fedha hizo za matumizi kwa mwaka uliopita ambapo jumla ya Tsh. 1,404,000,000 ziliombwa kwa matumizi ya tume kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi inasimamia Programu Kuu moja ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar yenye programu ndogo mbili; ya Uendeshaji wa Shughuli za Kiutawala wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Uendeshaji wa Shughuli za Kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Pemba.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI, ZANZIBAR

Mhe. Spika, jumla ya Tsh. 1,360,200,000 zinaombwa kwa kutekelezwa kwa programu kuu hii, ambapo jumla ya Tsh. 1,174,812,000 zinatarajiwa kutumika kwa programu ndogo ya uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar na Tsh. 185,388,000 zitatumika kwa prgramu ndogo ya pili ya uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi, Pemba.

Mhe. Spika, kamati yetu imeipitisha bajeti ya Tume ya Uchaguzi bila ya kufanya mabadiliko yoyote, tukiamini kuwa fedha hizo zitapatikana na kutumika ipasavyo na kuleta tija iliyokusidiwa. Aidha, kamati yetu imefuatilia zaidi katika kazi zake za usimamizi (*oversight*), ili kuona hali halisi ya utekelezwaji wa programu kuu na programu ndogo za Tume ya Uchaguzi.

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA KUDHIBITI DAWA ZA KULEVYA (FUNGU C04)

Mhe. Spika, serikali imekusudia kuanzisha Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na fedha za matumizi zinazoombwa kwa tume hii zitasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume. Aidha, tunakumbuka kuwa shughuli za kuratibu mapambano ya dawa za kulevya zilikuwa zinasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, tume hii itatekeleza programu kuu mbili; Programu kuu ya kwanza ni Udhibiti wa Dawa za Kulevya itakayokuwa na programu ndogo mbili;

programu ndogo ya udhibiti wa usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya na programu ndogo ya pili ni kinga ya msingi ya mahitaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Programu kuu ya pili ni ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya nayo ina programu ndogo mbili; programu ndogo ya utawala na uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya na programu ndogo ya pili ni Kuratibu Shughuli za Tume ya Dawa za Kulevya, Pemba.

PROGRAMU KUU YA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, programu kuu hii inaombewa jumla ya Tsh. 88,913,000 ambazo zitatumika kama ifuatavyo:

Shilingi 53,413,000 kwa programu ndogo ya Udhibiti wa Usambazaji wa Dawa za Kulevya, ambapo Tsh. 30,313,000 zitatumika kwa kudhibiti uingizaji na kudhibiti usafirishaji wa dawa za kulevya katika bandari rasmi na zisizo rasmi na Tsh. 23,100,000 zitatumika kwa kuzuia usambazaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili kwa programu kuu hii itatumia Tsh. 35,500,000 kwa ajili ya kinga ya msingi ya mahitaji na matumizi ya dawa za kulevya. Fedha hizo zitatumika kwa kuhamasisha jamii juu ya athari za dawa za kulevya kwa kutumia Tsh. 6,000,000 na fedha zilizobakia Tsh. 29,500,000 zitatumika kwa kujengea uwezo nyumba za upataji nafuu (*Sober House).*

PROGRAM KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA TUME YA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, programu kuu hii itatumia Tsh. 350,987,000 ambapo Tsh. 288,281,000 zitatumika kwa programu ndogo ya utawala na uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya, kwa kutumia fedha zote hizo kujenga uwezo wa wafanyakazi katika uratibu wa mapambano ya dawa za kulevya. Tsh. 62,706,000 zitatumika kwa programu ndogo ya pili ya kuratibu shughuli za Tume ya Dawa za Kulevya, Pemba.

Mhe. Spika,tume hii itawajengea uwezo wafanyakazi katika uratibu mapambano ya dawa za kulevya Pemba kwa Tsh. 56,591,000 na Tsh. 6,115,000 zitatumika kwa kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya katika bandari zisizo rasmi.

Mhe. Spika, kamati yetu imehoji haja ya kuanzishwa kwa tume hii, wakati kazi inazofanya ni kuratibu tu shughuli za kupambana na dawa za kulevya, bila ya kuwa na nguvu yoyote ya kisheria ya kuwachukulia hatua zozote za kisheria wahusika wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, kamati yetu ilitaka pia kufahamishwa mafanikio yaliyopatikana na changamoto wanazokabiliana nazo juu ya suala hili la uingizaji na matumizi ya madawa ya kulevya, ambapo tatizo hili bado linaendelea nchini mwetu. Vile vile, kamati iliiomba tume itoe maelezo ya kesi za madawa ya kulevya hasa *cocaine*, *heroine* na madawa mengine yanayoingizwa kutoka nje na matuhumiwa wangapi wamekamatwa na wamepatikana na hatia.

Mhe. Spika, kamati yetu ilijuulishwa kuwa, moja kati ya matatizo makubwa ya kuendelea kwa matumizi ya dawa za kulevya nchi ni rushwa, tena inahusishwa zaidi na Idara ya Mahakama na Jeshi la Polisi, kutokana na usiri juu ya kesi za madawa ya kulevya zinazowakabili watuhumiwa hao. Aidha, tatizo la madawa ya kulevya nchini ni kubwa na mara nyengine linawahusisha hata viongozi wa kidini na wafanya biashara wakubwa.

Mhe. Spika, kamati yetu inaendelea kuitaka serikali kutumia juhudi kubwa kwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kuwachukulia hatua kali zaidi wale wote wanaojihusishwa na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya.Serikali iendelee kuisimamia Sheria ya Kupambana na Madawa ya Kulevya, Sheria Nam. 9 ya mwaka 2009 na kuhakikisha pamoja na mambo mengine inadhibiti uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya nchini. Pia, kamati yetu inaishauri serikali kuangalia uwezekano wa mabadiliko ya sheria hii ili iendane na wakati na itoe adhabu kali zaidi kwa watakaopatikana na hatia.

Mhe. Spika, ushauri huu unatokana kwamba, vitendo vya uingizaji wa dawa za kulevya unaongezeka hapa nchini kwetu. Kwa hivyo, kamati inaishauri serikali kwamba, kulifanyia kazi rasmi suala hili kama vile inavyofanyia kazi matatizo mbali mbali yanayoibuka nchini mwetu, ili kuinusuru nchi yetu kuingia katika matatizo makubwa zaidi yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Mhe. Spika, kamati yetu inasisitiza na kuitaka serikali kuipa nguvu kubwa zaidi za kisheria na fedha za kutosha Tume hii ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya, ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi zaidi. Pia, Kamati inaamini kwamba, kama serikali itakuwa imara, tatizo la dawa za kulevya hapa kwetu litapungua au kumalizika kabisa.

TUME YA UKIMWI YA ZANZIBAR (FUNGU C05)

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI inahitaji jumla ya Tsh.1,205,876,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017, tofauti na Tsh. 1,703,500,000 zilizoombwa mwaka uliopita na hivyo kuwa na upungufu wa Tsh. 497,624,000 wa bajeti hizi mbili, kuliko sababishwa na Mpango wa Kubana Matumizi. Lakini kamati inaamini kiasi hiki kilichopatikana kwa serikali yetu kama kitatumika vizuri kinaweza kabisa kukidhi haja na matunda yake yakaonekana.

Mhe. Spika,Tume ya UKIMWI inatekeleza Programu Kuu mbili zenye programu ndogo mbili. Programu Kuu ya kwanza inahusu Uratibu wa Muitiko wa Taifa na UKIMWI yenye programu ndogo ya Mawasiliano na Utetezi na Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI. Programu Kuu ya pili ni ya Utawala na Uendeshaji yenye programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya UKIMWI Pemba na Utawala na Uendeshaji.

PROGRAMU KUU YA MUITIKO WA TAIFA NA UKIMWI

Mhe. Spika, programu kuu hii inaombewa jumla ya Tsh. 741,365,000 ambapo Tsh. 248,959,000 zitatumika kwa programu ndogo ya Mawasiliano na Utetezi kwa ajili ya kufanya uhamasishaji na utetezi ili kupunguza mazingira hatari ya *VVU* na kuchochea mabadiliko ya tabia kwa makundi maalumu ya jamii na Tsh. 492,405,000 zitatumika kwa programu ndogo ya Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI.

Mhe. Spika, kati ya Tsh. 492,405,000, Tsh. 50,185,000 zitatumika kwa kuelimisha jamii juu ya Sheria ya Kusimamia na kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2013 na haki za binaadamu; Tsh. 38,091,000 zitatumika kwa kuandaa Mkakati wa Tatu wa Taifa wa UKIMWI na Tsh. 404,129,000 zitatumika kwa kufanya ufuatiliaji na kuratibu shughuli za UKIMWI kwa Sekta za Serikali, Wilaya, Sekta Binafsi, AZAKI na Shehia.

PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

Mhe. Spika, jumla ya Tsh. 464,511,000 zimeombwa kwa ajili ya kutekeleza programu kuu hii, huku Tsh. 137,978,000 zitatumika kwa programu ndogo ya uratibu wa masuala ya UKIMWI Pemba, ambapo Tsh. 131,603,000 zitatumika kwa kazi ya kuweka mazingira mazuri ya kazi na Tsh. 6,375,000 zitatumika kwa uratibu wa masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika, programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Unguja iliyo chini ya Programu Kuu hii itatumia jumla ya Tsh. 326,533,000 kwa mwaka 2016/2017, huku Tsh. 286,957,000 zitatumika kuweka mazingira mazuri ya kazi, Tsh. 15,210,000 zitatumika kwa kujenga uwezo wa kwa wafanyakazi na Tsh. 24,366,000 zitatumika kwa kusimamia matumizi mazuri ya fedha, uwazi na uwajibikaji.

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI imepangiwa kutekeleza miradi miwili mikuu inayotekelezwa kwa pamoja na Umoja wa Kimataifa wa kusaidia kupambana na UKIMWI; Mradi wa Kufanya Uhamasishaji na Utetezi ili Kupunguza Mazingira hatari ya *VVU* na Kuchochea Mabadiliko ya Tabia kwa Makundi Maalum ya Jamii, unaotarajiwa kutumia jumla ya Tsh. 157,793,000, ambapo kati ya hizo, Tsh. 11,257,000 zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, fedha ambazo zote kwa pamoja zitatumika kwa kuandaa na kurusha vipindi vya redio na *TV* na Tsh. 146,536,000 ambapo fedha hizo zitatolewa na Shirika la *UNFPA*.

Mhe. Spika, mradi wa pili utakaotekelezwa na Tume ya UKIMWI ya Zanzibar ni Kufanya Ufuatiliaji na Kuratibu Shughuli za UKIMWI kwa Sekta za Serikali, Wilaya, Sekta Binafsi, AZAKI na Shehia, ambapo jumla ya Tsh. 8,743,000 zitatolewa na Serikali na Tsh. 352,540,000 zitatolewa kama Ruzuku ya Nje na Shirika la *UNFPA*.

Mhe. Spika, kamati yetu imeidhinisha maombi yote ya fedha za Tume ya UKIMWI kwa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo tukitaraji kuwa fedha hizo zitapatikana kama zilivyoidhinishwa na zitatumiwa ipasavyo. Kamati yetu itafuatilia kwa karibu na umakini zaidi matumizi sahihi ya fedha hizo kama zitakavyoidhinishwa na Baraza hili na baada ya kumalizika kwa mkutano huu wa bajeti.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba sasa nichukue fursa hii tena kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa mashirikiano mazuri na kufanya kazi kwa bidii. Kwa fursa hii naomba kuwatambua Wajumbe hao na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Seif Abeid - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Mjumbe
4. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Said Mohammed - Mjumbe
6. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Mjumbe

7. Mhe. Mussa Ali Mussa - Mjumbe
8. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi)- Mjumbe

Aidha, kamati yangu, Makatibu wa Kamati pia tunapenda kuwapongeza ambao ni:

1. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu
2. Ndg. Othman Ali Haji - Katibu

Mhe. Spika, nashukuru kwa mara nyengine na Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kunisikiliza na ninawaomba waipitie Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuisoma na kuielewa na hatimae waichangie na waipitishe.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Omar Seif Abeid Mwenyekiti wa Kamati wa kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe, muda tulionao utamtosha mchangiaji mmoja tu kwa jioni ya leo. Kwa vile nitapenda kwa heshima na taadhima sasa nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ili awe mchangiaji wa mwanzo kwa jioni hii ya leo. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kuanza kama ifuatavyo kwanza kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya siku hadi siku.

Lakini pia Mhe. Spika, niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele kwa kunipa ridhaa ya kuja katika Baraza hili kuwa Mwakilishi wao na naamini kwamba hawakufanya makosa, najua jimbo jipya lina mambo mapya. Kwa hivyo, kuna mahitaji mbali mbali itabidi niyaseme hapa na hususan Afisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndio inayochukuwa dhima ya nchi yetu nzima wizara zote za nchi yetu hii.

Mhe. Spika, kwanza natoa pole kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa mvua za masika zilizonyesha kipindi hichi na tunaamini kwamba Wazanzibari wengi wameathirika kutokana na mvua hizo. Lakini mimi nitasemea zaidi wananchi

wangu wa Jimbo la Kijitoupele ambao wameathirika sana na hadi leo bado wanayumba kwa mambo madogo madogo ambayo wameathirika kwenye vyoo na mambo mengine maji kuingia katika majumba yao na kupasuka hata kuta kwa baadhi ya nyumba.

Upande ulioathirika zaidi ni sehemu ya Bondeni Mwanakwerekwe meli nne, Tomondo, Meli Nne Uzi, Fuoni Nyumba moja, Bonde la Kijitoupele, wananchi wangu hawa kwa asilimia kubwa wamepata shida kubwa lakini ndio mambo ya Mwenyezi Mungu. Nitamuomba tu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais baadae tufanya mazungumzo angalau kwenda kuwafariji kwa njia yoyote, asitoe kitu lakini awaone kwa sababu hakupata nafasi hii kwa sababu mazingira yalikuwa yamekataa kutokana na maafa yaliyotoka sehemu mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi nitalolizungumzia kwanza suala muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Maendeleo katika nchi yanahitaji mambo mengi; yanahitaji barabara, umeme, maji, afya pamoja na elimu. Ukiyakusanya mambo hayo maendeleo yatakuwa yamepatikana. Kwa bahati nzuri katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuna maeneo yameelezwa kwamba umeme vijiji umeenda vizuri na mimi hilo naliunga mkono na asilimia kubwa nchi yetu sasa hivi inangara kwa umeme.

Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Spika, naomba tu kumwambia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuna eneo nitalizungumza sana kwa sababu watu sehemu wanaishi kama mazingira ya kimasikini sana ni Mwanakwerekwe, katika jimbo hili kuna eneo moja zito lina matatizo katika baadhi ya sehemu mbili kama hizi zifuatazo katika jimbo langu la Kijitoupele lakini naanzia Mwanakwerekwe.

Mhe. Spika, Mwanakwerekwe hadi leo wananchi huku Meli nne Uzi wanapata shida ya umeme, umeme unakuwa mdogo kiasi kwamba wanapatashida siku hadi siku. Niiombe serikali hili waliangalie kwa hali na mali ili wananchi wetu wafaidike. Lakini katika sehemu ambayo nitaizungumzia Kwarara huku ndiko kunakomatatizo makubwa zaidi hasa ukiangalia huku Kwarara Madina, ni jina kubwa sana Mhe. Spika. Lakini bado mpaka leo wananchi wetu wanamatatizo makubwa sana ya umeme. Huko Kwarara Madina Mhe. Spika, hadi kufika leo hakuna hata nguzo moja ya umeme ukiacha umeme wenyewe ndio haupo kabisa.

Kwa hivyo, naomba kabisa kwa kuwa umeme uko vijijini, juzi nilizungumza hapa uko Tumbatu kwa Mhe. Haji Omar Kheri, umeme uko katika kijiji cha Kisiwapanda, nashangaa Mkoa wa Mjini Magharibi tena jina la Madina kuwa hakuna umeme. Naiomba serikali Mhe. Spika, kwa nguvu zake zote tuwapatie

umeme wenzetu hawa ili wafaidike na mambo mbali mbali katika ulimwengu wetu wa kileo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, moja wapo ni suala la maji. Maji bila ya umeme hayapatikani kwa sababu ukichimba kisima bila ya *pump* utakuwa hupati maji. Kwa hivyo, naiomba serikali suala hili liangaliwe ili wananchi hawa nao wajisikie kwamba katika muelekeo wa leo kwamba tunajegemea tunaishi kutokana na wakati tuliokuwa nao.

Mhe. Spika, jengine sekta ya viwanda, nashukuru hotuba hii imesema vizuri tu kwamba serikali imejitahidi kuelekeza katika viwanda mbali mbali hasa tukiangalia kwamba viwanda vyetu vilivyojengwa vinawasaidia wananchi wetu na serikali kupata faida katika mapato yake. Lakini niseme tu kwamba mimi bado nina mawazo makubwa kama yafuatavyo nimuombe tu Mhe. Makamu wa Pili umefika wakati narudia tena niliwahi kuwa katika Baraza hili nikasema kwamba, Mwanza ziwa Victoria na kwengineko wanasafirisha samaki wa maji baridi na ajira nyingi zinatoka katika eneo hilo, lakini pia pato la nchi linaongezeka kutokana na samaki maji baridi.

Leo Zanzibar tumezungukwa na bahari katika pembe zote nne, kwa nini tushindwe kutafuta kiwanda cha maana cha samaki ili wananchi wetu wa Zanzibar wafaidike kutokana na pato hili. Naamini Mhe. Spika, kama tutajitayarisha vizuri, kama tutakuwa na miundombinu ya bahari yenyewe kwa kutumia vyombo vya kileo pato litapatikana na wananchi wetu wengi watapata ajira.(*Makofi*)

Mhe. Spika, leo sikitai samaki kutoka nje kuja hapa Zanzibar, lakini China wanatuletea samaki hapa kwetu Zanzibar, ni jambo la kusikitisha sana wakati kumbe sisi tulikuwa tutoe samaki tuwasafirishie wao huko nje. Naiomba serikali kwa hili vijana wetu wanataka ajira, vijana wetu wanataka nyenzo za kuvulia ili wapate pato na kujisaidia wao pamoja na serikali yetu ipate pato.

Mhe. Spika, naishukuru serikali yetu hii ya Zanzibar, Dkt. Ali Moh'd Shein na pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wametoa nyenzo mbali mbali za boti katika madiko mbali mbali au katika wilaya mbali mbali. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Spika, hadi leo zile boti ziliko hatuzijui, kama tulikuwa na nia tuwape wananchi wetu wafaidike nafikiri bodi zile labda zimeuzwa sehemu mbali mbali au zimepotea wapi, hatuzijui ziko wapi. Lakini hili nitaomba tu Mhe. Spika, labda tuje tupewe maelezo zile bodi ziko wapi na zinafaidisha kitu gani mpaka sasa hivi. Kwa sababu lilikuwa vijana wetu wapate ajira ili wajisaidie wao pamoja na pato la nchi. Lakini baada yake boti zile labda

zimefanyiwa miradi mingine ambayo hatuijui kwa sababu samaki bado tunaagizia kutoka China.

Naiomba serikali hili liangaliwe na tupate maelezo mazuri juu ya hukakikisha kwamba vijana wetu wanataka ajira kutokana na sekta mbali mbali hasa viwanda, Zanzibar narudia tena tumezungukwa na bahari, kama tutakuwa na viwanda viwili Unguja na Pemba basi tutakuwa tumepata ajira kubwa sana kwa vijana wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine sekta ya barabara naipongeza sana serikali kwa hili. Serikali imejitahidi kwa hali na mali kuwahikisha kwamba wananchi wake wa Zanzibar wanafaidika kutokana na barabara zetu kuu na barabara za ndani. Kila atakayesimama hapa ana wajibu wa kuhakikisha kwamba barabara zimejengeka vizuri na zinasaidia huduma mbali mbali.

Lakini pamoja na huduma hiyo, ninarudia pale pale naiomba serikali pamoja na kwamba bajeti inayosema kuna mambo ambayo yameandaliwa katika bajeti ijayo, hii tuliyokuwa nayo kwamba barabara ambayo hii ya kutoka Kwarara Meli Tano mpaka Kwarara Kwangulangwa mpaka Maungani, barabara hii itajengwa kipindi hichi. Lakini ningeomba Mhe.Spika, naiomba serikali kwa huruma zake wananchi wa maeneo hayo wanapata shida kubwa sana, daladala haziendi, wananchi wanatoka sehemu mbali huko Kwarara Madina ninakokutaja wanakuja hospitali kuu mjini, wanabebwa watoto kwa gari ya ng'ombe ilikuwa. Akitoka mzazi kwa gari ya ng'ombe. Sasa nishukuru tu kwamba tumejitahidi na Mbunge. Tumepiga *grader* barabara nzuri inapitika lakini tuna hofu ikija mvua sasa barabara itakuwa haipitiki. (*Makofi*)

Naiomba serikali itusaidie. Iwasaidie wananchi wetu ili nao wafaidike. Lakini ninaamini hili tutashirikiana pamoja na Mbunge na Mwakilishi na sisi tutachangia kama vile viongozi wa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, suala jengine nitalizungumza hapa kwa ufupi kabisa lakini nitaendelea baadae ni suala la Kipindupindu. Mhe. Spika, Zanzibar ina historia ya kupata Kipindupindu kwa muda mfupi sana. Lakini safari hii na katika hotuba ya Mhe. Waziri, imeeleza kwamba maradhi ya Kipindupindu yamechukua muda wa miezi kama saba au minane. Ni hatari.

Lakini mimi ningeshauri au ningetoa kama wazo ni kitu gani kilichosababisha hasa Kipindupinu kuwa kimezagaa kiasi kile kwa muda mrefu kuliko hivi. Wananchi wangu wamenipa salamu nizitoe hapa katika Baraza hili, wana hofu lakini wataalamu wa afya wataangalia *pampers* wanasema ni chanzo kimoja

wapo kinachosambaza maradhi ya Kipindupindu kwa haraka. Na sababu ya kusema hivyo. Zamani ilikuwa hakuna *pampers* lakini leo zimezagaa. Lakini kuna utaalamu wa *pampers* kuzitumia. Wengine wakishatumia, yaani wakishatoa haja yake kwa mtoto wanakwenda kutupa katika majaa ambayo inazagaa na siku za mvua ndiyo hatari inaenea. Hao manzi wanaochukua uchafu ule kueneza sehemu nyengine.

Hili ninatoa ushauri tu. Serikali iangalie chanzo na misingi ya kitu kilichosababisha Kipindupindu kwa muda mrefu ni kitu gani. Lakini wananchi wengi katika Jimbo langu la Kijitoupele wameniambia niwasemee suala hili. Wana wasi wasi na tatizo la *pampers* ni chanzo kikubwa cha kusababisha Kipindupindu katika nchi yetu. Kwa hivyo, wataalamu nimesema wafanye kazi yao na wao tena watatoa maamuzi baadae.

Mhe. Spika, ninajua kuna wafanyabiashara wengi wa *pampers* watalalamika. Lakini kwenye kuokoa maisha ya binaadamu usiogope, kwani uhai wa mtu una thamani kuliko biashara yako. Kwa sababu wewe mmoja au kumi na moja, wakifa watu wawili ni hasara humu katika maisha yetu ya binaadamu kwa jambo ambalo linaweza kuzuilika. Naiomba serikali iangalie hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna masuala mazuri yamezungumzwa kwamba Mhe.Makamu wa Pili wa Rais, ofisi yake hivi sasa imechukua dhima ya kuwa na watu wenye ulemavu kutoka Wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuja kwake, madawa ya kulevya pamoja na mambo ya ukimwi. Mimi nipongeze hili kwa dhati kabisa na niwaombe watendaji wote wa sehemu hizi wafanye kazi zao kwa ufanisi ili faraja ipatikane badala ya matatizo.

Mhe. Spika, watu wenye ulemavu ni watu ambao wanaathirika sana siku hadi siku. Hivi sasa tukitaka tusitake, asilimia kubwa ya wananchi wetu wanasumbuka kutokana na walemavu kupata mambo ambayo hayawahusu. Lakini wanalazimishwa wafanye bila ya kutaka. Naiomba serikali, sheria zipo lakini sheria zetu ziongezwe uwezo zaidi kuhakikisha anayemdhalilisha mlemavu, hiyo inakuja kama na watoto na wazee au wanawake. Kwa sababu mlemavu hana hatia, mtoto mdogo hana hatia, mwanamke hana hatia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, leo tumesikia kwenye kipindi cha "Mawio". Kuna akina mama wetu wanalalamika huko mitaani. Kuna kikundi kimetokea katika sijui katika eneo gani, wanavamia nyumba za watu usiku, wanalazimisha mambo ambayo hayatakiwi kwenye jamii. Hivyo, naiomba serikali iwe kali sana kutokana na sheria zetu tunazotunga. Mtu anayefanya kosa la kubaka au mtoto au mwanamke, wapewe adhabu ambayo itastahiki hata kifunguo cha maisha,

tumsahau jela. Vyenginevyo, Mhe. Spika, mtu kamdhalilisha mlemavu, mwanamke au mtoto mdogo asiyekuwa na hatia, anakwenda anaambiwa aah! kafanya kosa fulani miezi mitatu jela. Akitoka anaanza upya. Akipigwa miaka kumi au miaka thalathini. Ninafikiri itakuwa somo zuri na jamii yetu itaishi kwa salama na amani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunaosikiliza taarifa Tanzania Bara kwenye vyombo vya habari katika Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma kuna watu wanajiita "Teleza". Hao wanakwenda kama walivyozaliwa. Mungu atunusuru yasije kwetu hapa. Wanakwenda katika majumba ya watu wanavamia kama alivyozaliwa, ukimkamata kateleza kakimbia. Kwa hivyo, hili ni somo moja wapo la kujihadhari na watoto wetu, kujihadhari na walemavu wetu pamoja na akina mama. Akina mama ndiyo wanaopata shida.

Mimi Ali Suleiman Ali (Shihata) kidogo nikisimama popote ninaweza kupapatua kwa njia yoyote ile. Lakini mama siku nyengine utazidiwa. Lakini wamo majasiri kuliko akina baba. Lakini siyo wote. Kwa hivyo, akina mama mwanzo wa huruma ni akina mama, halafu wanakuja na watoto wetu, halafu wanakuja walemavu wetu. Tuwaweke katika lengo ambalo la kusitiri maisha yao ya kuhakikisha kwamba wanaishi salama katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine nitakalolizungumza hapa ni suala la rushwa. Bahati nzuri Mhe. Spika, taarifa ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kalizungumzia uzuri udhibiti wa mambo ya rushwa kwenye maeneo yetu. Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar alipolizindua Baraza hili alisema kuwa atahakikisha kama Tanzania kuna usemi umesema, Rais wa Muungano wa Tanzania atatumbua majipu na anayatumbua kweli kweli majipu. Yeye kasema vipi "Jipu likishatumbuliwa kama halikutolewa moyo litarudi". Kwa hivyo, huu moyo aliouhakikisha Mhe. Rais, yanapotokea matatizo tusimuonee aibu mtu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, uchumi wa nchi unategemea usimamizi mzuri kama ninavyosema kila siku. Ukimuonea aibu yule anakwenda kukusanya mapato au anayekwenda kutia ulaghai wa kitu fulani ili apate yeye, hatwendi. Nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Wewe ndiyo mtendaji mkuu wa serikali. Nikuombe kwa dhati kabisa. Kila muhujumu wa aina yoyote tusimpe fursa katika nchi yetu. Akiwa mtalii, mfanyabiashara, ikiwa mtu yeyote wa aina yeyote anahatarisha pato letu la nchi tusimpe nafasi. Vyenginevyo, Mhe. Spika, tumesema asilimia kubwa ya bajeti yetu tutajitegemea na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kama tutakusanya mapato tunaweza kujitegemea bila ya matatizo. (*Makofi*)

Niombe tusimamie, tusionane aibu, tusimuonee huruma mtu yeyote. Hata kama mtoto wa Shihata. Kafanya kosa Mhe. Spika, tuhakikishe tunamuadhibu kutokana na kosa lake. Mhe. Spika, hili linawezekana na kuwezekana kwake ni kusimamia. Kusimamia ni uaminifu wa watu wetu, wawe waaminifu katika sehemu hizi. Vyenginevyo, rushwa itaendelea siku hadi siku. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini pia watu wanauliza hii rushwa kama mimi nimekwenda pahala nimeambiwa Mhe. Shihata, ninakupa rushwa ninataka kitu fulani au umemuona mtu anatoa rushwa. Sasa ende wapi. Wenzetu Tanzania Bara wanatoa mpaka nambari za simu. Likitokea tatizo piga nambari fulani bure. Na hapa ninaomba tuweke kitengo hicho wananchi wetu waelewe. Vyenginevyo, mambo haya yatakuwa yanaendelea siku hadi siku.

Mhe. Spika, ni athari za pato la nchi. Limo katika mikono yetu. Athari za pato la nchi linatakiwa usimamizi mzuri ili pato lipatikane. Katika biashara kuna mambo mawili; kununua na kuuza. Sasa kama mfanyakazi kauza biashara yake. Umekwenda kununua vitu leo shilingi milioni tano au laki moja tu, hata shilingi elfu ishirini usiidharau, dai risiti. Risiti ni chanzo kimoja wapo cha kukusanya mapato yetu na bila ya risiti Mhe. Spika, hatuna mapato tutakayoyapata. (*Makofi*)

Kwa hivyo, niombe somo hili liendelezwe kwa ajili ya wananchi wetu walielewe faida na hasara. Faida kutaka risiti upewe. Lakini pia Mhe. Spika, ninaamini kama tutatoka hapa tutakwenda katika maeneo mbali mbali, ninakuhakikishia baadhi ya maeneo mengi wafanyabiashara hawana vitabu vya risiti kabisa. Ukimwambia aah! mimi kitabu sijui nimekiweka wapi. Siyo utaratibu. Hivyo, tuwaambie wenzetu ambao wanaohusika na mambo ya risiti wawe tayari kwenda kukusanya kwa wakati wowote ili wananchi wetu wafaidike na mambo hayo.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna mambo mengine ambayo yanatuhangaisha katika maeneo yetu. Mhe. Spika, umefika wakati hivi sasa katika baadhi ya maeneo yetu vitendo vya hujuma vinaendelea. Na ninasema tu kwamba vitendo vya hujuma vipo vya aina nyingi; Wizi wa nguvu unaingia katika maeneo yetu, watu wanavamiwa katika nyumba zao na watu hao wanaonekana lakini bado kila tukiwaweka katika hatia, inakuwa bado haijafikiwa.

Ningeomba sana serikali hili suala hili lieleweke na liendelezwe kuwaokoa wananchi wetu ambao wanasumbuka siku hadi siku. Mitaa mingi hivi sasa Mhe. Spika, haya yapo na yanaendelea. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, yeye ni Mkuu wa Shughuli za Serikali aendelee

kuhakikisha kwamba wanaohusika na mambo ya kusimamia shughuli hizi, wasimamie kwa jumla ili kuhakikisha wananchi wanaishi katika amani na utulivu kwenye nchi yao.

Mhe. Spika, niishukuru Tume ya Uchaguzi. Naishukuru kwa dhati kabisa pamoja na matatizo yaliyojitokeza.Niseme tu kwamba unapokwenda kucheza mpira kuna mambo mawili au matatu, lakini mawili kwanza; kushinda, kushindwa na *draw* ambalo hilo ni la tatu. Lakini mimi ninakiri kwamba kushinda na kushindwa uje na mchezo safi na wa halali. Lakini mchezo ikiwa haukwenda *fair*, inakuwa si mchezo. Rifarii anaweza kusema hata akakataa na akavunja mpira wakati wowote.

Mimi ni mshabiki wa *Simba Sport Club*. Tena ni mwanachama hai. Lakini sina nongwa. Nikifanya vibaya ninakiri nimefanya vibaya. Nikifanya vyema nimefanya vyema. Ninaipongeza Yanga kwa kuchukua ubingwa. Lakini naipa pole kwa kundi lilopangwa, ninaitakia heri ishinde lakini sijui mbele itafikaje. (*Makofi*)

Mhe. Spika, maana ya kusema hivyo, kuna mchezo na alikuwa rifarii Mhe. Hafidh Ali, sisahau maisha yangu nilikua katika Uwanja wa Taifa. Mhe. Hafidh Ali, Simba toka hawajaingia uwanjani wanasema hatumtaki. Lakini akalazimishwa lazima achezeshe. Tunakwenda kila wakati, akiingia kwenye *zone* mchezaji anaambiwa ata *off side*, sijui nani. Ikabidi Mhe. Spika, mpira ule mara ya pili kurudiwa kwenye mchezo ule, mchezo haukurudiwa tena, tukakataa kuingia uwanjani, tumefahamiana eeh! Lakini tumekataa kuingia uwanjani wenyewe kwa sababu tulijuwa tumeshindwa, tumefahamiana eeh! Nimejua tumeshindwa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, niseme tu kwamba Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanya kazi yake vizuri na marudio ilikuwa ni kwa vyama vyote. Waliokataa walijua kama Shihata timu ya Simba imeshindwa. Hivyo, mchezo ulimalizika hapo Mhe. Spika. Lakini niseme tu Mhe. Spika, Tume yetu ya Uchaguzi mimi ninaipongeza na kwa dhati kabisa, imefanya kazi vizuri. Lakini matokeo yaliyojitokeza haya ni ya kibinadamu na lazima yatafutiwe ufumbuzi mzuri ili kuweka vizuri huko mbele tunakokwenda. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine nitazungumzia kijumla jamala. Mhe. Spika, hivi sasa tunaingia katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwezi Mtukufu wa Ramadhani wananchi wetu wanategemea mahitaji mbali mbali ya kupata riziki yao ya kununua kwa njia yoyote ya halali. Lakini bado kuna tuhuma, siyo

sahihi, kuna tuhuma kwamba wafanyabiashara wanaonekana hawapo tayari safari hii kuingiza futari katika nchi yetu.

Ningeiomba serikali hili likaangaliwa kwa hali na mali. Wazanzibari tumebahatika soko letu lipo Tanzania Bara. Tanzania Bara tunapata kila kitu. Mimi ninawashukuru wenzetu. Wanatuunga mkono kwa asilimia mia moja. Unaweza ukasikia Mkoa fulani una kasoro ya chakula, sisi hapa mchele tunao, maharagwe tunayo na kila kitu tunacho. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili liangaliwe wafanyabiashara wetu waliokuwa si waaminifu, wanataka kuleta kidogo vurugu *match* hapa. Tuwe tayari kukabiliana nao kwa hali yoyote.

Asubuhi lilikuja suala hapa. Je, tunajiandaa vipi na Ramadhani kesho kutwa. Kwa hivyo, niseme tu kwamba Mwenyezi Mungu akitujaalia Mhe. Spika, tunategemea kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu kwa salama na amani katika nchi yetu na wananchi wetu wanufaike na bidhaa inayotoka Bara kuja hapa. Mara nyingi tunapata nazi kutoka Bara, maharagwe yanatoka Bara, mbatata zinatoka Bara. Kwa hivyo, nimuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili azungumze na wafanyabiashara waaminifu kwa moyo safi kabisa. Wananchi wasije kukosa mahitaji ya lazima katika mwezi wa Ramadhani. Tunaamini muhogo tunapata kwetu, ndizi tunapata si haba, lakini kuna mahitaji mengine ya lazima yanatoka Tanzania Bara. Hivyo, niseme hili ninakuomba Mhe. Spika, liangaliwe kwa manufaa ya watu wetu wote.

Mhe. Spika, jengine hili litakuwa ni la mwisho kabisa. Katika maisha yetu ya kila siku kuna masuala ambayo yanawagusa watu mbali mbali. Na watu mara nyingi huwa wanategemea huduma hizi za jamii. Ninakwenda kwenye sekta ya afya, hii ninaizungumzia kwa jumla.

Mhe. Spika, tunaishukuru Wizara ya Afya, tunawashukuru madaktari wetu na wauguzi. Lakini bado kuna malalamiko. Kuna malalamiko hospitali bado uangalizi wake si mzuri kwa wananchi wetu, wanapata usumbufu mkubwa. Leo inaweza kutokea ajali na Mwenyezi Mungu atuepushie au kama mama mja mzito. Wengine wanalalamika humu. Wanaweza kwenda hospitali wakatukanwa mpaka wakajuta Mhe. Spika. Kwa hivyo, niiombe serikali kwa kuwa tunakwenda katika utawala bora na utawala bora ni kuhudumia jamii ipasavyo. Naiomba serikali wauguzi, madaktari wetu wamekwenda pale kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi wetu. Ikiwa anataka kazi aendelee na kazi, hataki kazi, ndiyo jipu lenyewe Mhe. Spika. Hilo ndilo jipu lenyewe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na hii kama utataka kupata taarifa za kila siku, ninaahidi utaipata kila siku taarifa. Naomba sana madaktari wetu ninawapenda na wauguzi kwa sababu wanakumbana na kazi nzito kwenye maeneo yetu. Lakini ninaiomba serikali iwe kali kutokana na usumbufu wanaoupata wananchi wetu siku hadi siku.

Lakini kwenye hapo hapo la mwisho nitazungumzia Kipindupindu kwa wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika eneo la Chumbuni la Mhe. Miraji. Maana Mhe. Machano Othman Said, kahama lakini yupo pale pale na yeye.

Mhe. Spika, kuna malalamiko haya ninayatoa hadharani na Waziri wa Afya atayachukua. Kuna wafanyakazi Mhe. Spika, wamenituma siwataji majina, siyo utaratibu. Hawa wamesema kwamba wamefanya kazi katika mazingira magumu na sisi tunakiri sote kuwa wamefanya katika mazingira magumu. Maana kama utapata siku ukenda siku moja tu ukaambiwa uingie pale ndani huingii. Wao walijitolea usiku na mchana, wameacha kila yao. Lakini Mhe. Spika, hadi leo baadhi hawajalipwa. Naiomba serikali kwa hili. Maana kama askari kenda vitani yule. Askari akenda vitani akirudi na mimi nilikuwa mwanajeshi bahati nzuri. Sikuwahi kwenda Uganda lakini nilikuwa *standby* wakati wowote.

Mhe. Spika, baada ya vita Mhe. Rais Nyerere alisema, "Sina la kuwapa isipokuwa ahsante". Lakini wanajeshi tunatii tulikubali. Lakini mfanyakazi mwengine atakuwa kidogo kinyume na mwanajeshi, waliokwenda vitani waliorudi. Maana sote tulikuwa *standby* pamoja lakini tuliambiwa hatuna la kuwapa isipokuwa ahsante. Sasa mimi ninaomba ahsante ya wale watu wetu madaktari na wauguzi wagaiwe chochote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninaiomba serikali kwa dhati kabisa watu hawa wafikiriwe, wagaiwe chochote angalau wawe na nguvu huko mbele tunakokwenda. Naomba lisitokee tena na tunamuombe Mwenyezi Mungu maradhi haya hasije tena katika nchi yetu na ayapeperushe sehemu ya nchi yetu yasitukaribie. Lakini wafikiriwe na wagaiwe posho lao. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa heshima kabisa na taadhima ninaiunga mkono hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kaisoma kwa unyenyekevu na uzito mzima. Na mimi ninaiunga mkono pamoja na wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali, kwa kutufungulia wachangiaji kwenye Ofisi hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Waheshimiwa Wajumbe, nina matangazo mawili. Kwanza nimeombwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar, anawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kutoka Pemba wakutane katika ukumbi wa juu mara baada ya kuahirishwa kwa Baraza.

Tangazo la pili, linahusu semina kesho. Naomba nikutangazieni Waheshimiwa Wajumbe kwamba ile semina haitokuwepo tena. Na sababu kubwa ni kwamba baadhi ya wenzetu watakuwa hawapo na tuliwahitaji nao ni washiriki ili sote tuweze kushiriki. Kwa hivyo, semina hiyo itapangiwa wakati mwengine, kesho haitokuwepo. Mutautumia muda wenu ninafikiri kwa ajili ya kupanga mambo yenu mengine.

Waheshimiwa, jambo jengine la mwisho nililonalo kwenye orodha yangu ya walioomba kuchangia ukimtoa Mhe. Ali Suleiman Ali, ambaye amemaliza kuzungumza sasa hivi, nina wachangiaji kumi na nne ambao wameomba. Ofisi hii tunataka siku ya Jumatatu jioni wawe wanahitimisha hii hoja yao.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 58(6) inasema kwamba;

> "Kila Mjumbe anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika ishirini wakati wa mikutano ya kawaida na dakika thalathini wakati wa mikutano ya bajeti, lakini Spika akiona inafaa anaweza kumuongezea msemaji dakika si zaidi ya kumi".

Waheshimiwa, mimi nilikuwa na ombi la kwamba tupunguze, siyo kwamba nizidishe ile kumi lakini huu muda wa dakika thalathini ukimuacha Mhe. Ali Suleiman Ali, ambaye amefaidika kwa sababu ameutumia wote. Wanaokuja kuanzia Jumatatu basi tukubaliane ili iwe nusu ya huo muda ili wapate kuchangia walio wengi. (*Makofi*)

Lakini ili tulitimize hilo nitamuomba sasa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atupe hoja au Mwanasheria Mkuu ili tuweze kuiamua. Mheshimiwa, tafadhali.

HOJA YA KUTENGA KANDO KANUNI YA 58(6)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiye mwenye hoja hapa iliyoko mbele, sasa akisema yeye ataonekana ana *interest* ya kupunguza muda.

Lakini kama ambavyo umesema Mhe. Spika, naomba nitoe hoja ya kutenga kando Kanuni ya 58(6) ambayo inayoongoza michango katika Kikao cha Bajeti ili tutenge kando kanuni hiyo na muda wa kuchangia uwe ni dakika kumi na tano badala ya thalathini.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu, hoja imetolewa na naona imeungwa mkono, sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, hoja ni kutengua kanuni ya 58(6) ili sasa muda badala ya dakika 30 iwe dakika 15. Wale Waheshimiwa Wajumbe wanaounga mkono wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabisa nitangulize shukurani zangu za dhati kabisa kwa kutolewa hii hoja na namna ambavyo mumeiunga mkono. Kwa hivyo, tutakuwa tunachangia kwa muda wa dakika kumi na tano. Na ni vizuri watu wajiandae vizuri kwa sababu waliozoea kuchangia nusu saa, wanaweza wakajikuta muda wao unamalizika na yale mambo yao ya muhimu bado hawajazungumza.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hoja hiyo kuamuliwa. Sasa naomba kwa heshima na taadhima, niahirishe shughuli za Baraza mpaka siku ya Jumatatu tarehe 30/05/2016, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1:41 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 30/05/2016 saa 3:00 asubuhi)